# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Novemba 7, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581487

nipasheTZ nipasheTZ

0745 700710 LIKE & FOLLOW US

The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital

epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com





UKURASA 21

**GUARDIOLA ATAKA NYOTA WENYE HASIRA**

# Kilio mikopo elimu ya juu

• **Walalama** ni 'kiduchu', haiendani na mahitaji ya vyuo; yatima wa TASAF akwama nyumbani... *Ukurasa 3*



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru

UKURASA WA 5

**India** yazindua chuo Zanzibar, kujenga Hospitali ya Apollo Bara





UKURASA WA 4

**Walimu** walioadhibiwa kwa wimbo wa Zuchu watetewa bungeni



UKURASA WA 19

**Waisrael** waigawa Gaza pande mbili



UKURASA WA 3

## DED AKAMATWA, APELEKWA KIGOMA

JESHI la Polisi Mkoa wa Tabora limemkamata Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga mkoani humo, Athumani Msabila kwa tuhuma...

## Deni la Serikali lafika Tril. 82/-

UKURASA 2



Ndivyo hali ilivyokuwa jana asubuhi katika usafiri wa treni ya daladala, abiria waliokosa nafasi kutokana na hali ngumu ya usafiri, walipanda sehemu zisizoruhusiwa kufanikisha safari yao, kituo cha Ukonga Madafu- Mombasa, Dar es Salaam. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**



## Adha ya usafiri, abiria waning'inia hadi kwenye kichwa treni Dar

UKURASA 4

**MICHEZO** **SIMBA WATOA SABABU KUKUBALI KIPIGO** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Deni la Serikali lafika Tril. 82/-

**Na Gwamaka Alipipi,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema hadi kufikia Juni mwaka huu, Deni la Serikali lilikuwa ni Sh. trilioni 82.1.

Amesema fedha za deni hilo zimetumika kugharamia miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme, elimu na afya.

Alitoa kauli hiyo jana bungeni alipowasilisha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25.

Dk. Mwigulu alisema tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Desemba 2022 inaonesha limeendelea kuwa himilivu katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

Waziri huyo alisema mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 4.6 katika mwaka ulioishia Juni mwaka huu ambao ulibakia ndani ya lengo la nchi na mtangamano wa kiuchumi kikanda.

Alisema mfumuko wa bei kwa kipindi cha Julai hadi Septemba 2023 ulikuwa wastani wa asilimia 3.3 kulinganishwa na asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2022.

Dk. Mwigulu alisema mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 22.2 kwa mwaka 2022/23 kulinganishwa na lengo la ukuaji la asilimia 10.7.

Alisema ukuaji huo umeongezeka kulinganishwa na ukuaji wa asilimia 9.9 mwaka 2021/22, kwamba ukuaji huo unaakisi ongezeko la mahitaji ya mikopo mipya kwa sekta binafsi kutokana na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi zilizokuwa zimeathiriwa na janga la virusi vya corona.

Alisema jitihada zinazoendelea kutekelezwa na serikali katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji na utekelezaji wa sera wezeshi za fedha na bajeti.

Dk. Mwigulu alisema mikopo chechefu ilipungua kufikia wastani wa asilimia 5.3 Juni 2023 kutoka asilimia 7.8 Juni 2022.

Alisema akiba ya fedha za kigeni imeendelea kukidhi mahitaji ya fedha za kigeni kwa ajili ya uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi.

Alisema hadi kufikia Juni 2023, akiba ya fedha za kigeni ilikuwa Dola za Marekani bilioni 5.45 kulinganishwa na Dola bilioni 5.11 Juni 2022.

Alisema kiasi hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4.9.

"Kiwango hiki ni zaidi ya lengo la nchi la kukidhi miezi minne na zaidi ya lengo la miezi 4.5 kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki," alisema Dk. Mwigulu.

Dk. Mwigulu alisema mwaka 2022/23, kampuni ya Moody's Investors Service Ltd na Fitch Rating Services Ltd zilifanya tathmini ya uwezo wa nchi kukopesheka na kuchapisha matokeo ya daraja B2+ na B+, mtawalia.

**BAJETI IJAYO**

Katika hatua nyingine, serikali inatarajia kukusanya na kutumia Sh. trilioni 47.4 kwa mwaka wa fedha 2024/25. Kati yake, Sh. trilioni 34.4 ni mapato ya ndani (72.6%), washirika wa maendeleo wanatarajiwa kuchangia Sh.trilioni 4.2 (9% ya bajeti).

Vilevile, serikali inatarajia kukopa Sh. trilioni 6.1 kwa mwaka wa fedha 2024/25 kutoka soko la ndani na Sh. trilioni 2.5 kutoka soko la nje.



Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Waziri Mwigulu alitoa taarifa hiyo jana bungeni, akisema matokeo ya bajeti ya serikali ya mwaka 2024/25 yamezingatia mwenendo wa ukusanyaji mapato, matarajio ya ukuaji wa uchumi, hali ya uchumi wa dunia na mikakati ambayo serikali inaendelea kuchukua katika kuongeza mapato ya ndani kama ilivyoainishwa kwenye sehemu ya pili ya mwongozo.

Alisema matumizi ya serikali yanakadiriwa kuwa Sh. trilioni 47.4 mwaka 2024/25. Kati yake, Deni la Serikali ni Sh. trilioni 12.1, mishahara Sh. triloni 11,7 na uendeshaji wa shughuli za serikali Sh. trilioni 8.2.

Dk. Mwigulu alisema matumizi kwa ajili ya programu na miradi ya maendeleo ni Sh. trilioni 15.3 ikijumuisha ruzuku ya maendeleo (elimumsingi na sekondari bila ada na mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu).

"Makadirio haya yamezingatia mahitaji ya kugharamia deni la serikali; mishahara ya watumishi wa umma; uendeshaji wa miradi iliyokamilika ikiwamo miundombinu ya elimu, afya, umeme na maji; ugharamiaji wa uchaguzi wa serikali za mitaa na maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025," alisema.

Dk. Mwigulu alisema baadhi ya mikakati itakayotumika katika kufikia lengo la makusanyo ya mapato ya ndani ni pamoja na kutanua wigo wa ukusanyaji mapato kwa kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuhakikisha vyanzo hivyo vinaakisi misingi ya ukusanyaji mapato.

Dk. Mwigulu alisema Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25 umeainisha maelekezo ambayo maofisa masuuli wanapaswa kuyazingatia wakati wa uandaaji, utekelezaji na ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti.

Aliyataja maelekezo hayo ni wakati wa utekelezaji bajeti ya mwaka 2024/25 hakutakuwa na bajeti ya nyongeza ambayo itatengwa na Wizara ya Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za fungu ambazo hazikutengewa bajeti.

Lingine ni maofisa masuuli kutakiwa kutoa kipaumbele katika kutenga bajeti ya kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuibua miradi mipya.

**MAENEO YA KIPAUMBELE**

Serikali pia imeainisha maeneo ya kipaumbele katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 ambayo ni kuchochea kasi ya ukuaji uchumi jumuishi, kupunguza umaskini, kuzalisha ajira na kutengeneza utajiri na kuchochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alitaja vipaumbele hivyo jana bungeni wakati akiwasilisha mapendekezo ya mpango wa taifa kwa mwaka 2024/25.

Prof. Kitila alisema katika kufikia shabaha hiyo, msukumo utawekwa katika kuongeza tija ya uzalishaji na uongezaji thamani katika sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini.

Alisema msukumo pia utawekwa katika kuchochea na kuboresha ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote; kuongeza na kuimarisha matumizi zaidi ya teknolojia, hususani Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA); kuongeza uzalishaji viwandani na kuimarisha huduma bora za jamii kwa wote.

**MALENGO YA JUMLA**

Prof. Kitila alitaja malengo ya jumla ya mpango huo mojawapo ni kuendelea kulinda mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano iliyopita.

Lengo lingine ni kuendelea na mikakati ya kujitosheleza kwa mahitaji ya chakula nchini kwa kuendelea kuongeza matumizi ya mbolea, mbegu bora na kilimo cha umwagiliaji.

Alitaja lengo lingine ni kuongeza uzalishaji na uuzaji wa bidhaa (pamoja na huduma) nje ya nchi kupitia sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini.

Lingine ni kuweka mkazo wa pekee katika kuongeza thamani katika mazao yanayozalishwa kupitia sekta za kilimo, ufugaji, uvuvi, misitu na madini.

Prof. Kitila alitaja lengo lingine ni kuendelea kuongeza, kuboresha na kuimarisha ubora wa huduma za jamii, ikiwa ni pamoja na elimu, afya, maji na umeme.

Lengo lingine Waziri Mkumbo alilitaja ni kuendelea kupanua na kuimarisha miundombinu ya usafiri wa barabara, reli, anga na majini pamoja na utunzaji endelevu wa mazingira.

Alitaja lengo lingine ni kujielekeza kwenye kufungua fursa katika sekta za madini ya kimkakati, uvuvi wa bahari kuu, uchumi wa kijani na uchumi wa kidigitali.

Prof. Kitila alisema: "Maeneo haya matatu ni yanayokamata kasi duniani kwa sasa na ambayo kwa upande wetu hatujavuna ipasavyo."

Alisema wananchi wengi nchini (65.1% ya idadi ya watu wote Tanzania), wanaishi vijijini na kwamba shughuli nyingi za uzalishaji zinategemea kilimo.

Alisema sekta ya kilimo imeajiri asilimia 61 ya nguvu kazi na kwamba kasi ya ukuaji wa uchumi vijijini haiendi sambamba na kasi ya ukuaji wa uchumi mijini.

Prof. Kitila alisema ukuaji wa sekta ya uzalishaji viwandani unategemea malighafi kutoka maeneo ya vijijini.

"Izingatiwe pia kwamba mifumo ya ugharimiaji wa shughuli za kiuchumi haishikamani na shughuli za kilimo vijijini (ambapo mikopo yote ya kibiashara nchini ni Sh. trilioni 22, wakati mikopo inayokwenda katika sekta ya kilimo ni asilimia saba pekee).

"Hivyo basi, ninapendekeza kuwa katika mipango yetu ijayo ya maendeleo tuweke mkazo maalum katika kuhakikisha kuwa uchumi wa vijijini unakuwa sehemu muhimu ya uchumi wa taifa," alisema.

**HATUA ZITAKAZOCHUKULIWA**

Prof. Kitila alisema katika kuchochea na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii vijijini, serikali itachukua hatua mbalimbali ikiwamo kuendelea kuwawezesha wakulima kuongeza uzalishaji.

Alisema: "Tutaendelea kuwapatia wakulima wadogo mbegu bora na mbolea kwa bei ya ruzuku na kuendelea kupanua na kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji."

Waziri huyo pia alisema wataweka mazingira maalum katika kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini na kuendelea kupanua na kuboresha miundombinu ya huduma za afya, elimu, maji, na umeme.

Alisema watahakikisha kuwa angalau asilimia 30 ya wananchi vijijini wanakuwa na bima ya afya ifikapo mwaka 2025, kuimarisha ubora wa elimu hususani kuhakikisha shule za vijijini zina walimu wa kutosha na kuunganishwa katika miundombinu ya kidijitali.

**WAWAKEZAJI**

Prof. Kitila alisema mwaka ujao serikali itaweka mkazo katika kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza na kuimarisha ujazo wa fedha za kigeni.

Alisema kwa kuzingatia hali ya ushindani duniani katika kuvutia uwekezaji, serikali itachukua hatua mbalimbali katika kuvutia uwekezaji wa kimkakati na uongezaji wa thamani wa mazao mbalimbali.

Alitaja hatua hizo ni kuweka mkakati wa kulenga masoko makubwa ya nje ili kuwezesha uzalishaji wa bidhaa kwa tija na ushindani.

Hatua nyingine ni kutoa msukumo wa pekee katika kuvutia uwekezaji katika ujenzi wa viwanda vya nguo, kuanzisha mtaa wa sayansi, teknolojia na dijitali kwa ajili ya kuchochea na kuibua ubunifu na ugunduzi unaohitajika katika mapinduzi ya nne ya viwanda.

Pia alisema serikali itaweka mazingira mahususi kwa lengo la kuvutia wawekezaji watakaokuwa tayari kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya madini hususani katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha betri za magari na mitambo.

Alitaja mkakati mwingine ni kuweka mkazo katika utekelezaji miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa katika ukuaji wa uchumi na ile inayoiwezesha nchi kutumia fursa za wakati.

# Kilio mikopo elimu ya juu nchini

**Na Waandishi Wetu**

BABA yake alifariki dunia miaka 10 iliyopita. Sasa anaishi na bibi yake kijijini Mishepo, wilayani Shinyanga, wakitegemea msaada wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), huku ngazi ya safari yake aliyoiwekea mikakati ikivunjika.

Ndoto yake ya kuwa Ofisa Maendeleo ya Jamii na Usafi wa Mazingira na Maji inaonekana kuchelewa kutimia na huenda isitimie baada ya Bodi ya Mkopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kumpangia mkopo 'kiduchu' kwa ajili ya elimu juu.

Huyo ni Godfrey Mbogo (21), mhitimu wa kidato cha nne mwaka 2020 wa Shule ya Sekondari ya Kata ya Mwantini wilayani Shinyanga. Sasa ameachwa kwenye giza nene, kushindwa kujiunga na Chuo cha Maji Dar es Salaam mwaka huu alikochaguliwa.

Kijana huyo licha ya kutimiza vigezo na masharti yote ya kitaaluma kukidhi matakwa, shida imejitokeza upande wa ufadhili unaotokana na mkopo.

HESLB imempangia mkopo wa Sh. 230,000 kati ya Sh. milioni 1.35 zinazohitajika kwa ajili ya ada ya masomo chuoni huko.

Katika mazungumzo na Nipashe jana wilayani Shinyanga, Mbogo, akionesha taarifa alizotumiwa kupitia mfumo wa mikopo wa HESLB, alisema bodi imempangia mkopo wa Sh. milioni 2.47 kwa mwaka huu wa masomo kwa ajili ya posho ya kujikimu na Sh. 230,000 kwa ajili ya ada ya masomo.

"Masomo yameshaanza, lakini nimelazimika nikae nyumbani (kijijini Mishepo). Nitajaribu tena kuomba mkopo mwakani. Unaona mwenyewe familia yetu ilivyo hapa, bibi hana uwezo wa kunilipia fedha zote hizi zinazohitajika.

"Ada tu ninatakiwa nilipe Sh. 1,350,000 (milioni 1.35), lakini bodi wamenipangia Sh. 230,000, wamenipangia 'boom' (posho ya kujikimu) lakini sijapewa fedha ya vitabu, mafunzo kwa vitendo, utafiti.

"Hapo kuna mahitaji mengine; chuoni ukifika wanataka ulipe 300,000 ya gharama zingine, kuna bima ya afya Sh. 50,400. Hicho chuo nimeambia hakina mabweni. Nitatoa wapi fedha za kutosheleza mahitaji yote hayo?" Mbogo alilalama.

Katika ufuatiliaji wake, mwandishi alibaini kuwa kijana huyo amefaulu kwa daraja la kwanza, akipata alama nane katika mchepuo wa HGL katika matokeo ya Mtihani wa Kidato cha Sita (Shule ya Sekondari Sengerema) mwaka huu.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa kijana huyo, mwanafunzi wa mwaka katika Chuo Kikuu cha Tumaini (TUDARCo), Happyfania Michael ana kilio kinachofanana na cha Mbogo.

Mzaliwa huyo wa Moshi mkoani Kilimanjaro alisoma katika Shule ya Sekondari Makongo na baadaye kusoma kidato cha tano na sita mkoani Mtwara kwenye Shule ya Wasichana Nangwanda.

"Wazazi wangu wote wapo hai, mama yangu ni mama wa nyumbani na baba ni anajishughulisha na biashara ndogondogo.

"Cha kusitikisha bodi (HESLB) imenipatia Sh. 2,590,000 kwa ajili ya 'boom' na Sh. 110,000 kwa ajili ya vitabu. Fedha kwa ajili ya ada sijapangiwa ambayo zaidi ya milioni 1.9/- kwa mwaka," alilalama.

Alisema kinachompa matumaini kuendelea kuwa na subiri, ni fursa ya kukata rufani kupinga kiwango cha mkopo alichopewa.

Mwanafunzi wa mwaka wa kwanza anayesoma ngazi ya shahada katika stadi ya ualimu chuoni huko (TUDARCo), Helena Pius, amepangiwa mkopo sawa na Happyfania.

Walisoma shule moja kidato cha tano na sita (Nagwanda Girls), wazazi wake wote wako hai, ni wafanyabiashara ndogondogo, lakini naye hajapangiwa mkopo kwa ajili ya ada, utafiti na masomo kwa vitendo.

"Kuna gharama mbalimbali za maisha kama usafiri, chakula na mambo mengine yanayohusu chuo ukizingatia ada yangu ni Sh. 1,850,000. Ni kiwango kikubwa sana kwa wazazi wangu kukimudu," alisema.

Naye Hamis Mihambo, mwanafunzi wa mwaka wa kwanza katika Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) anadai amepangiwa mkopo wa Sh. 60,000 kwa ajili ya vitabu na Sh. milioni 2.64 kwa ajili ya posho ya kujikimu, lakini hajapangiwa fedha kwa ajili ya ada ambayo ni Sh. milioni 1.2 kwa mwaka, mafunzo kwa vitendo, utafiti na mahitaji maalum ya kitivo chake.

**KAULI YA HESLB**

Ofisa Elimu na Uhusiano wa HESLB, Omega Ngole, alipotafutwa jana kuzungumzia malalamiko hayo, alisema mikopo ya elimu ya juu inatolewa kulingana na maelezo yaliyotolewa na mwombaji.

Alisema mwanafunzi yeyote ambaye hajaridhika na mkopo aliopewa, anaweza kukata rufani kuanzia wiki hii.

"Ni kama mimi na wewe tukienda hospitalini kutibiwa, tukapimwa na wote tukakutwa na malaria, mimi tatu wewe moja, ni wazi kwamba dozi zetu zitakuwa tofauti," alisema.

Ngole alisema kuwa baadhi ya wanafunzi wanaolalamika kuwa ni yatima na wamekosa mkopo hawakujaza vizuri fomu ya maombi ya mkopo. Alisema kipaumbele ni wenye ulemavu, waliofadhiliwa masomo ya sekondari kutokana na wazazi wao kukosa uwezo na yatima.

"Kuna mwingine anakuambia yeye ni yatima kwa mdomo, lakini ukiangalia maombi yake hajajaza hilo. Tumeunganisha maombi yetu na Wakala wa Usajili wa Vizazi na Vifo (RITA), ambao unathibitisha vyeti vya vifo.

"Tunafungua dirisha la rufani wiki hii. Mtu ambaye anaona hajaridhika, anawasilisha ombi lake la rufani la kuongezewa kwa kuweka tena nyaraka sahihi kama hakuweka mwanzo," alisema Ngole.

HESLB ilianzishwa rasmi kisheria mwaka 2005 ikiwa na majukumu makuu mawili; kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa elimu ya juu na kukusanya mikopo iliyoiva ambayo imetolewa na serikali tangu mwaka 1994/1995.

## DED atiwa mbaroni, apelekwa Kigoma

**Na Thobias Mwanakatwe**

JESHI la Polisi Mkoa wa Tabora limemkamata Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga mkoani humo, Athumani Msabila kwa tuhuma ambazo hazijawekwa wazi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Richard Abwao, jana alithibitisha kukamatwa kwa mkurugenzi huyo juzi mchana na amesafirishwa kupelekwa mkoani Kigoma.

"Ni kweli mkurugenzi huyo tulimkamata, lakini siwezi kutoa maelezo zaidi sababu ya kukamatwa kwake kwani baada ya kumkamata tumempeleka mkoani Kigoma alikokuwa anafanya kazi awali kabla ya kuhamishiwa Igunga ambako ndiko ana kesi," alisema.


Kamanda Abwao alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Kigoma ndilo linaweza kutoa ufafanuzi zaidi sababu za kukamatwa kwake kwa kuwa ndiko alifanya kosa akiwa mtumishi huko.

Taarifa kutoka Igunga zilieleza kuwa mkurugenzi huyo alikamatwa Novemba 5 mwaka huu mchana muda mfupi baada ya kurejea kutokea mkoani Dodoma ambako alikwenda kikazi.

Pamoja na sababu za kukamatwa kwa mkurugenzi huyo kutowekwa wazi, baadhi ya viongozi wa mikoa ya Tabora na Kigoma wamedai huenda ni matokeo ya uchunguzi wa kamati iliyoundwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa ambayo ilikabidhi ripoti yake Oktoba 25 mwaka huu jijini Dodoma.

Waziri Mkuu Majaliwa alipokea taarifa hiyo ya uchunguzi wa tuhuma za ubadhirifu wa fedha kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji. Ilibainika kuwa watu 10 wanahusika na mtandao wa uhamishaji fedha kinyume cha taratibu.

Akipokea ripoti hiyo, Waziri Mkuu alisema kila mtumishi wa umma ni lazima atunze na kuratibu vizuri matumizi ya fedha. Aliagiza hatua za haraka za kishera zichukuliwe dhidi ya wahusika wote.



Rais Samia Suluhu Hassan akizungumza na Katibu Msaidizi wa Umoja wa Mataifa anayeshughulikia masuala ya Kibinadamu na Naibu Mratibu wa Huduma za Dharura, Joyce Msuya, Ikulu Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

## PURA yaokoa bil. 189/- utafiti mafuta

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) imeokoa Sh. bilioni 189 kwa kufanya ukaguzi wa kina wa hesabu za kampuni zinazojihusisha na utafiti na uzalishaji kwenye sekta za mafuta na gesi nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Charles Sangweni, alisema hayo jana katika kikao kazi cha mamlaka hiyo, wahariri na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, uliondaliwa na Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mashirika yaliyo chini yake kuelezea umma, shughuli wanazofanya, mafanikio na changamoto.

Sangweni alisema PURA iliokoa kiasi hicho tangu kuanza kutekeleza majukumu yake mwaka 2015.

"Kama tusingefanya ukaguzi huu haya mapato yasingekuwapo. Lakini baada ya kuamua kufanya wenyewe, tumeokoa kiasi hiki cha fedha. Mfano hizi kampuni tangu tumeingia walikuwa wazungu tu, PURA tukaingilia. Tungependa Watanzania wakapata kama wao badala ya kujiajiri," alisema.

Mafanikio mengine, alisema ni baadhi ya kampuni kumaliza mikataba yao, waliishauri serikali kuziongezea na kuendelea na uwekezaji katika sekta hiyo.Akizungumzia kuhusu magari kuanza kutumia gesi, alisema zaidi ya magari 2,000 jijini Dar es Salaam yamefungwa mfumo.

"Uzuri wake umbali ambao ungetumia lita moja ya gesi ya Sh. 1,550 kama lita moja ya petroli inauzwa Sh. 4,500 unakuwa umeokoa Sh. 3,000," alisema.

Sangweni alisema magari hayo yalianza kufungwa mfumo huo hivi karibu katika vituo maalumu vilivyowekwa jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo, alisema wanahitaji vifunguliwe vituo vingi vya kujaza gesi kwenye magari na kurahisisha upatikanaji wa huduma hiyo.

Alitaja faida nyingine ya magari kutumia gesi kuwa ni kuondokana na uchafuzi wa mazingira. Alisema ufungaji wa mfumo huo ulianza nchini kutokana na bei ya mafuta kupanda, hivyo kumpunguzia mmiliki wa gari gharama kubwa ya mafuta ambayo yamekuwa yakipanda mara kwa mara kwa sababu mbalimbali.

Awali, alisema serikali inaendelea kufanya jitihada za makusudi za kutafuta mafuta nchini ili kuhakikisha Tanzania inaachana na utegemezi wa kupata nishati hiyo kutoka nje.

"Ndiyo maana tuna mradi wa bomba la mafuta kutoka Tanzania hadi Uganda. Jitihada za Tanzania kutafuta mafuta nchini zilianza miaka 50 kwa ushirikiano wa Bara na Visiwani.

"Utafutaji wa mafuta ni gharama kubwa sana ndiyo maana tuna wataalamu waliobebea katika fani hii," alisema.

Pia alisema katika utafiti wao wamegundua kuwapo kwa viashiria miamba tabaka 534,020 nchini na kwamba wanaendelea kufanya utafiti kwa kuangalia dunia kuhusu athari za mazingira kutokana na uchafuzi wa mazingira.

Alisema kampuni nyingi zinazokuja nchini zinaingia mkataba kabla ya kuanza na baada ya kupata mafuta na kwamba baada ya kufanya utafiti, mafuta kama yatapatikana wanaingia mkataba wa kugawana mapato.

"Mkataba tunaingia na yule anayechimba, akipata tunakaa kubaliana jinsi ya kugawana mapato na akikosa tunampa mkono wa kwaheri," alisema.

# Adha usafiri, abiria waning'inia hadi kwenye kichwa treni Dar

**Na Christina Mwakangale**

MVUA inayoendelea nchini siku ya tano, kwa Dar es Salaam imeibua adha ya usafiri huku wanaotumia usafiri wa treni, maarufu kama 'Treni ya Mwakyembe' abiria wamelazimika kuning'inia katika mabehewa hadi kwenye kichwa.

Ni hatua ambayo haijashuhudiwa tangu kuanzishwa kwa usafiri huo kwa Shirika la Reli Tanzania (TRC).

Ugumu huo unatokana na kukosekana kwa daladala za kutosha kama ilivyozoeleka, huku tayari barabara ya Nyerere, kati ya Kariakoo na Gongo la Mboto, ikiwa katika ujenzi wa usafiri wa mwendokasi.

Hiyo ndiyo hali inayotawala katika usafiri wa aina hiyo, unaohudumia na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), kuanzia Stesheni Kuu iliyoko Buguruni hadi Pugu Mwakanga. Zote zinatoza nauli ya Sh. 600.

Nipashe ilikuwapo jana saa 3:00 asubuhi katika stesheni ya TRC - Mombasa, Ukonga, Dar es Salaam ambako treni iliyokuwa ikitoka Pugu Stesheni Kwenda Relwe Gerezani, ilikuwa imejaza abiria wengine wakining'inia nje ya milango iliyofungwa, kuzuia watu kuingia kwa kuwa kulikuwa kumejaa.

Hata hivyo, umati wa abiria walikuwapo hapo walikimbilia kuning'inia milangoni katika mabehewa hayo 18 na wengine wakakimbilia kwenye kichwa cha treni, walikopanda wake kwa waume pembeni hadi sehemu aliko dereva.

Ni hali iliyofanya treni hiyo kusimama kwa muda, huku dereva akiingiza baadhi ya abiria katika chumba chake, wengine wakiwa sehemu ya mbele hata kumzuia kuona vizuri.

Katika usafiri wa TAZARA ambako Nipashe ilikuwako pia, umati wa abiria waliofurika katika vituo mbalimbali, nao walikwama baada ya kupita kiberenge kikiwa na tangazo kwamba 'treni imebuma' abiria waking'aka.

Ndiyo hali iliyotawala Alhamisi wiki iliyopita, treni ya TRC iliyopaswa kuondoka Relwe Gerezani saa 2:15 usiku ilianza safari saa 3:00 mahali hapo kukifurika abiria katika namna ambayo haijazoeleka.

Kimsingi, tangu mchana siku hiyo hali ya usafiri ilikuwa mbaya, magari yalikuwa machache, yamejaa abiria na hayaendi, usafiri kati ya Gongo la Mboto na Kariakoo, unaochukua wastani wa saa moja ilikuwa zaidi ya saa nne.

Abiria mmojawapo, Jasmine Petro, aliiambia Nipashe alivyokwama kwenda kazini kuwa: "Leo hakufai foleni kubwa sana na wanakojenga barabara ya mwendokasi, maji yamejaa. Nimepanda gari Mombasa (Ukonga) saa 4:30 asubuhi hadi Vingunguti nimeshuka nimetumia saa tatu.

"Nimeshuka Vingunguti kurudi nyumbani nimetumia saa mbili. Sasa ndio naingia ndani (hiyo ikiwa saa 10:16 jioni). Nimetumia saa mbili ndani ya gari. Magari hayatembei.

Simulizi kama hizo, Nancy Mushi, mkazi wa Kunduchi Salasala, mwenye usafiri binafsi anaisimulia Nipashe kuwa adha ya kutoka mtaani kwake hadi barabara ya Bagamoyo kwenye lami, ambako ana mazoea ya kutumia dakika 10, imemgharimu zaidi ya dakika 45.

Mzigo wa adha hiyo, ndio mwandishi ameshuhudia kwa wanafunzi baadhi wa kidato cha pili, ambao wako katika mitihani ya kitaifa tangu Jumatatu iliyopita na wanamalizia leo, wamekuwa wakiteseka na wengine kutembea kwa miguu, kwenye mvua kuwahi mitihani shuleni.

Mwanafunzi anayeishi Ukonga-Mombasa, aliyejitambulisha kwa jina moja la Peter, anayesoma katika shule ya sekondari iliyoko Kitunda Mwanagati, wastani wa kilomita saba, alisema amekuwa akitumia pikipiki huku akilowa, hali inayomgharimu zaidi ya Sh. 8,000 kwa siku, kumudu ratiba ya mitihani na mvua.

Kwa mujibu wa tovuti ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), mvua hizo zinabashiriwa kuendelea hadi Ijumaa wiki hii.

Kimsingi. Hiyo ndiyo picha iliyotawala takribani kona zote za mkoa wa Dar es Salaam, mvua zilivyodhibiti nyendo za watu kutafuta riziki na safari za wanafunzi.



Kituo cha daladala zinazofanya ruti ya Segerea, Gongo la Mboto na Tandika kupitia Barabara ya Malamba Mawili, kilichopo Mbezi Mwisho Manispaa ya Ubungo, kikiwa kimeharibika kutokana na mvua inayoendelea kuonyesha jijini Dar es Salaam. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Spika Tulia aingilia kati walimu kuvuliwa vyeo 'Honey' ya Zuchu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SAKATA la walimu wawili wa shule mbili za msingi zilizoko Tunduma mkoani Songwe kusimamishwa na kuvuliwa madaraka kwa kile kinachodaiwa kushindwa kusimamia maadili ya wanafunzi kwa kuwaruhusu kucheza wimbo wa 'Honey' wa Zuchu, limetinga bungeni.

Uongozi wa Bunge umeitaka serikali kuwarejesha kazini walimu hao na kuwapa nafasi ya kusikilizwa.

Hatua hiyo imetokana na Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Husna Sekiboko akichangia hivi karibuni mjadala bungeni, kuhoji kuhusu nyimbo zinazostahili kupigwa wakati wa taasisi za elimu na hatua zinazopaswa kuchukuliwa kwa wanaokiuka.

Mbunge huyo aliitaka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kutoa mwongozo wa nyimbo zinazostahili kupigwa na zisizostahili shuleni.

Alidai kuwa kuna taarifa kuwa walimu hao walisimamishwa wakiwa nje ya vituo vya kazi.

Akitoa maelezo ya ziada kuhusu suala hilo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson aliitaka serikali kutoa mwongozo wa aina ya muziki inayoruhusiwa kupigwa shuleni wakati wa shughuli mbalimbali.

"Kama ni kweli walimu hao hawakuwapo shuleni wakati mamlaka ya nidhamu inachukua hatua, warejeshwe katika nafasi zao na kama walikuwapo mamlaka iendelee na utaratibu wake.

"Hauwezi kuwasimamisha halafu ukataka wakate rufani ndipo wajieleze kuwa hawakuwapo shuleni. Ilipaswa hatua zichukuliwe kabla," alisema.

Dk. Tulia alisema wapo mawaziri bungeni na wabunge huwa wanacheza muziki na wanafunzi na kwamba kuna video zipo zinaonesha hilo.

"Ni muhimu mwende na hatua zaidi ya hapa ili watu wote wawe wanaelewa ni muziki gani inachezwa, ipi haichezwi itasaidia sana hilo liwe hatua ya pili.

"Sasa ama tutarudi nyuma au tutaanzia hapa ili watu wajue nini cha kufanya, la sivyo tutaendelea kucheza huo muziki watoto wakiwa shuleni halafu tutawaponza wale ambao watatakiwa kuchukuliwa hatua," alielekeza.

Aliagiza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambayo ina jukumu la kumshauri Waziri wa Elimu, kuangalia suala hilo kwa umakini bila kuchanganya imani ya dini na maadili.

"Angalieni huko nyimbo zipi zinaruhusiwa na zipi haziruhusiwi ili tusiingie mtego wa kwamba aliyecheza si mbunge. Kwa hiyo, anaadhibiwa mwalimu... mazingira hayo yataleta mkanganyiko," alisema.

Awali, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda alisema serikali ina jukumu la kusimamia malezi shuleni, kudhibiti aina ya muziki unaoruhusiwa shuleni na kukataza muziki unaokiuka maadili ya Kitanzania.

"Mfano, muziki unaokatazwa ni unaochochea masuala ya ngono, pombe au sigara. Kamishna wa Elimu amesisitiza hata katika mabasi muziki unaopigwa uzingatie maadili hayo.

"Ni muhimu kutambua kuwa si kila kitu kinachokubaliwa uraiani kinakubaliwa shuleni; kwamba pombe inaruhusiwa huko haina maana shuleni inaruhusiwa.

"Inawezekana kuna muziki mwingine uraiani unaonekana wa kawaida, haina maana kwamba unaruhusiwa shuleni. Sisi tuna wajibu huo wa kusimamia mambo hayo na wazazi wanafanya hivyo.

"Ninatoa wito kusisitiza kwamba wote ambao wanasimamia shule wahakikishe wanadhibiti kile kinachotumika kama muziki shuleni ili tusikiuke suala la maadili," alifafanua.

Waziri huyo alisema suala la nidhamu, kama walimu hao hawakuwapo shuleni, wana nafasi ya kukata rufani kwa mkurugenzi aliyewaondoa katika nafasi zao.

Baada ya maelezo hayo, ndipo Spika Tulia alisema hatua za nidhamu zina pande mbili, hivyo aliyekosea ana haki ya kusikilizwa.

"Kama taarifa za kusema walikuwamo ama hawakuwamo mimi na wewe tunao uwezo wa kufanikisha tusiseme sasa, lakini kama mamlaka ya nidhamu imechukua hatua kabla ya kujua kuhusu hilo ilipaswa isikilize hilo. Mimi ninajua ndio mnavyofanya, au mnachukua hatua bila kuwasilikiza?" alihoji.

Akijibu hoja hiyo, Prof. Mkenda alisema alisisitiza kuwa kama walichukuliwa hatua bila kusikilizwa, inapaswa wakate rufani na ni utaratibu mzuri wa kushughulikia suala hilo.

Baada ya maelezo hayo, Mnadhimu Mkuu wa Shughuli za Serikali Bungeni, Jenista Mhagama, aliomba agizo hilo likutanishe taasisi zinazohusika zilizopewa mamlaka ya kusimamia masuala yote ya nidhamu kwa watumishi na sekta hiyo ya elimu ili kuhitimisha kwa kutumia taratibu zilizopo na kila mmoja atendewe haki.

# India yazindua chuo Zanzibar, kujenga Hospitali Apollo Bara

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHUO cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na Uvumbuzi cha India (IIT Madras), kimefungua tawi Zanzibar, huku Rais Dk. Hussein Ali Mwinyi, akisema hatua hiyo imetimiza ndoto aliyokuwa nayo.

Amesema tangu anagombea urais wa Zanzibar katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 alikuwa na ndoto ya kuifanya Zanzibar kuwa kituo kikuu cha vyuo vikuu kutoka nchi mbalimbali duniani.

Wakati Dk. Mwinyi akisema hivyo, Hospitali ya Apollo pia ya India inatarajia kujenga tawi lake jijini Dar es Salaam.

Akizindua kampasi ya chuo hicho jana wakati wa kuweka jiwe la msingi kampasi ya kudumu ya Bwelea, Fumba nje ya mji wa Zanzibar, alisema taasisi hiyo inatoa wahandisi waliobobea katika teknolojia na uvumbuzi wanatumika katika nchi mbalimbali duniani.

Dk. Mwinyi alisema lengo kuu la serikali kwa kushirikiana na serikali ya India kuanzisha kampasi ya chuo hicho ni kuleta maendeleo ya nchi na watu wake kielimu, kiuchumi na kijamii.

"Ilikuwa ndoto yangu. Sikuwahi kufikiria chuo hiki ndicho cha kwanza ambacho kitakuja Zanzibar kwani ni miongoni mwa vyuo vikuu bora duniani. Naamini vyuo vingine vingi vitafuata kuja kuanzisha matawi yao hapa nchini," alisema Dk. Mwinyi.Alisema serikali kwa makusudi imeamua kuanzisha kampasi hiyo, kuharakisha utekelezaji wa mipango yake na kufikia maendeleo yanayotarajiwa ili kufikia dira ya maendeleo ya 2050 kuweka zaidi katika kuwatayarisha wafanyakazi wenye taaluma na ujuzi.

Alisema hawawezi kufanya mageuzi ya kiuchumi bila ya kuwa na wataalamu watakaoenda sambamba na dunia, hivyo kuweko kwa kampasi hiyo Zanzibar ni hatua moja kubwa ya kutayarisha mazingira bora ya kufanikisha utekelezaji wa dira hiyo.

"Hivi sasa Zanzibar, Tanzania na Afrika kwa ujumla ina uhitaji mkubwa wa wataalamu wa teknolojia ambao watasaidia kukabiliana na changamoto za kimaendeleo zilizopo na mageuzi yanayofanywa na serikali katika mitaala ya elimu, lengo ni kuwawezesha wanafunzi kutumia ujuzi walioupata kwa vitendo," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema uanzishwaji wa kampasi hiyo utazisogeza karibu fursa za kupata wataalamu ambao watatumika katika viwanda ubunifu na miundombinu katika nchi na bara la Afrika kwa ujumla.

Katika hatua nyingine, serikali imeingia makubaliano ya kudumu na Hospitali ya Apollo kuanza kutoa huduma bobezi za kibingwa nchini zenye kuzingatia teknolojia za kisasa.

Kujengwa kwa hospitali hiyo ni matokeo ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyoifanya nchini India Oktoba 11 mwaka huu baada ya kufanya mazungumzo na Hospitali ya Apollo.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Dk. John Jingu, wakati akizungumza na waandishi wa habari alieleza makubaliano yao hospitali hiyo itajengwa ndani ya miaka mitatu iwe imekamilika na kuanza kutoa huduma.

Alisema Rais Samia alikutana na uongozi wa hospitali za Apollo nchini India aliwaomba waone uwezekano kuja kuweka hospitali ya kisasa Tanzania.

Alisema uwekezaji wa hospitali hiyo ni juhudi za Rais Samia katika kuhakikisha Tanzania inakuwa ni kituo cha umahiri katika utoaji wa tiba Afrika hususani ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Alisema baada ya Rais Samia kukutana nao walianza mazungumzo na viongozi wa hospitali na kuja nchini kwa ajili ya kuangalia eneo la kuweleza hospitali hiyo itakayojengwa Dar es Salaam.

"Wamekuja kutembelea maeneo mbalimbali ambayo watawekeza hospitali hiyo tumetembelea maeneo mbalimbali ya Dar es Salaam kuna maeneo yamewavutia wanaendelea kuyafanyia kazi ili kuwekeza hospitali ya kisasa yenye teknolojia za kisasa," alisema.

Dk. Jingu alitaja faida ya uwekezaji huo utasaidia kuboresha huduma za afya kwa sababu wanakuja na teknolojia mpya na kusababisha ushindani katika sekta hiyo.

"Hii hospitali itasaidia kuleta ushindani kwa taasisi ama hospitali ambazo zipo wakati mwingine kama hakuna ushindani huduma zinaweza zisiwe nzuri. Tunaamini ushindani huo utasaidi kuongeza tija, ufanisi katika utoaji wa matibabu, huduma na kuboresha huduma za afya nchini," alisema.

Dk. Jingu alisema uwekezaji huo utaleta chachu kubwa katika uchumi wa nchi na itasaidia kupunguza gharama ya kusafirisha watu kwenda kutibiwa nje ya nchi.

Alisema faida nyingine ni kupunguza fedha za kigeni kwenda nje ya nchi kwa kuwa zimekuwa zikitumika nyingi wanapokuwa wanawatibu wagonjwa ng'ambo.

"Ajira za moja kwa moja ziatakuwa nyingi na mafunzo kwa kuwa tumekubaliana moja ya mambo wanayotakiwa kuyafanya ni kuwajengea uwezo wataalamu wa nchini katika maeneo mbalimbali ili huduma zinazotolewa ziwe shindani za kimataifa," alisema.

**•Imeandikwa na Rahma Suleiman, ZANZIBAR na Beatrice Shayo, DAR.**




Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa tatu kulia) akiwa na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Mohamed Mussa pamoja Balozi wa India Nchini, Binaya Srikanta Pradhan (kushoto), wakifungua pazia kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi la ujenzi wa Taasisi ya Teknolojia ya Madras (IIT) Kampasi ya Zanzibar, Fumba Wilaya ya Magharibi "B" Mkoa wa Mjini Magharibi jana. Wa pili kulia ni mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi. **PICHA: IKULU**


twiga cement
HEIDELBERGCEMENT Group

## TANZANIA PORTLAND CEMENT PUBLIC LIMITED COMPANY

## UNAUDITED RESULTS FOR THE PERIOD ENDED 30 SEPTEMBER 2023

### CHAIRMAN'S STATEMENT

(TPCPLC) continues to deliver strong operating results. The Company has experienced a stable growth in revenue compared to the same period in 2022. Revenue and operating profit grew by 5% year on year.

This good performance is attributed to process improvement and cost control in our production. Plant availability and efficiency also played a vital role to the improved performance in 2023.

The Company continues to focus on customer service and selling new products within our high quality portfolio. We maintain strong customer reationships which enabes TPCPLC to demonstrate its strength as the eading payer in the industry.

**Prospects**
In spite of the cement demand growing slowly this year, we are optimistic about the months to come. TPCPLC will continue to work on improving efficiency and operating performance.

**Appreciation**
The Board would like to thank all its stakeholders for their support. We have every confidence that TPCPLC will continue to deliver value for the shareholders and community in the future.

**BY ORDER OF THE BOARD**

Hakan Gurdal
Chairman of the Board

**STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE PERIOD ENDED 30 SEPTEMBER 2023**

| TZS '000 | 2023 | 2022 |
|---|---|---|
| Revenue from contracts with customers | 375,403,916 | 358,338,268 |
| Cost of sales | (251,952,856) | (241,743,405) |
| **Gross profit** | **123,451,060** | **116,594,863** |
| | | |
| Other operating income | 3,037,218 | 1,584,600 |
| Selling and marketing expenses | (2,222,695) | (2,205,913) |
| Administrative expenses | (18,667,508) | (15,564,513) |
| Other operating expenses | (2,323,607) | (2,088,469) |
| **Operating profit** | **103,274,468** | **98,320,568** |
| | | |
| Finance income | 1,905,838 | 1,922,847 |
| Finance costs | (463,960) | (788,188) |
| Net gain on foreign currency translation | 6,574,990 | 1,077,009 |
| **Profit before tax** | **111,291,336** | **100,532,236** |
| | | |
| Income tax expense | (34,046,752) | (30,564,898) |
| **Profit for the period** | **77,244,584** | **69,967,338** |

**STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 30 SEPTEMBER 2023**

| TZS '000 | 2023 | 2022 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| **Non-current assets** | | 142,224,344 |
| Property, plant and equipment | 134,368,874 | 861,623 |
| Intangible assets | 866,726 | 987,893 |
| Leasehold land | 960,047 | 5,166,423 |
| Right of Use assets | 1,836,697 | 754,000 |
| Other financial assets | 592,000 | |
| | **138,624,344** | **149,994,283** |
| Current assets | | 74,386,616 |
| Inventories | 99,717,618 | 53,445,499 |
| Trade receivables | 60,672,251 | 18,659,144 |
| Other short-term operating receivables | 11,266,190 | 450,000 |
| Other financial assets | 300,000 | 89,219,635 |
| Cash and cash equivalent | 113,897,818 | |
| | **285,853,877** | **236,160,894** |
| | | |
| **TOTAL ASSETS** | **424,478,221** | **386,155,177** |
| | | |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | |
| Equity | | |
| Authorised, issued and fully paid-up share capital | 3,598,462 | 3,598,462 |
| Retained earnings | 303,215,188 | 268,434,562 |
| **TOTAL EQUITY** | **306,813,650** | **272,033,024** |
| | | |
| **Non-current liabilities** | | 5,378,124 |
| Lease liabilities | 2,063,777 | 5,754,887 |
| Employment benefit liabilities | 5,910,228 | 4,012,078 |
| Provision for quarry site restoration | 5,008,340 | 9,808,603 |
| Deferred income tax liability | 8,637,432 | |
| | **21,619,777** | **24,953,692** |
| **Current liabilities** | | |
| Lease liabilities | | 982,398 |
| Current income tax payable | (513,511) | 85,212,720 |
| Trade and other payables | 93,428,265 | 2,973,343 |
| Dividend payable | 3,130,040 | |
| | **96,044,794** | **89,168,461** |
| **TOTAL LIABILITIES** | **117,664,571** | **114,125,872** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **424,478,221** | **386,155,177** |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tutumie tamasha kubadili mambo

**MAFANIKIO** ya kuwa taifa lenye usawa wa kijinsia na fursa sawa kwa wote hayawezi kupatikana 'kiulaini' kama ilivyo mvua au jua.

Ni lazima kuwe na harakati zinazohusisha kazi za wadau, serikali, asasi za kiraia na vyombo vya habari mahiri vinavyojikita kupigania haki za raia wote na kukuza ushiriki wa wanawake katika maendeleo.

Mambo hayaishi hapo ni lazima kuwapo na majukwaa na mijadala yenye ubunifu ya kuboresha masuala ya usawa wa baina ya wanawake, wanaume, vijana na watoto kama Tamasha la Kitaifa la Jinsia linaloanza leo jijini Dar es Salaam.

Tunaupongeza Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa kuandaa jukwaa ambalo ni njia mojawapo ya kuhakikisha kuwa kizazi cha sasa kinahimiza wanawake na vijana kushiriki vyema katika masuala yote yanayohusu maendeleo ya nchi kwa faida ya sasa na kizazi kijacho.

Wiki hii kuanzia leo hadi Alhamisi TGNP na wadau wanashangilia mafanikio ya wanawake na uhimilivu wao katika kujisimamia, kujitetea, kujisemea na kukabiliana na changamoto zinazowakabili, kupitia tamasha hilo la Kitaifa la Jinsia.

Tunawapongeza , kwa ushiriki wa kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa wanawake. Wamefanya kile wanachosema na kufuatilia utekelezaji kwa lengo la kuboresha hadhi ya mwanamke na makundi ya wanyonge wa taifa hili.

Hongera TGNP kwa kufanikisha kampeni ya kuongeza uwezeshaji wa wanawake kiuchumi, uwakilishi wa kisiasa, kupigania kuboresha huduma za afya, maji na kufuatilia mitiririko ya bajeti katika mrengo wa kijinsia.

Ndiyo maana uwepo wa tamasha hili tunaona kama ndiyo wakati wa kuyatafakari na kuyapekua masuala yote haya ili watetezi wa wanawake waone kama kuna mafanikio.

Tunaona kuwa huu ndiyo wakati wa kujibu maswali, je, ahadi zinazotolewa na serikali na wadau zinatimizwa? Ni ukweli kuwa kuandaa sera, sheria na taratibu bora kumebadilisha au kumerekebisha mambo?

Hivyo, ni wakati wa kulitumia jukwaa la Tamasha la Kitaifa la Jinsia kuchunguza na kupata majibu na ikiwezekana kuwasikia viongozi na watendaji serikali wakitaja mafanikio yaliyofikiwa.

Tunaungana na wanaharakati kuwa juhudi zimefanyika lakini bado kuna ukosefu wa uwakilishi wa kutosha wa wanawake bungeni, wenyeviti wa halmashauri, madiwani kwenye taasisi mbalimbali kama wakuu wa vyuo vya elimu, vikuu na katika nyanja nyingi.


Tunaendelea kupongeza jitihada zinazofanyika lakini tunatamani kuona mambo yakiboreshwa zaidi ili tufikie 50/50 kwenye chaguzi za serikali za mitaa 2024 na 2025.

Tunaamini kuwa jukwaa hili linaloshirikisha wadau kutoka nje na ndani ni 'darasa' lenye ripoti za kitafiti zinazofafanua utekelezaji wa ahadi za kuinua kina mama na watoto wa Tanzania.

Tunafahamu kuwa kuna mengi ya kufahamu kwa mujibu wa tafiti kama hali ya unyanyasaji wa kijinsia au ubaguzi dhidi ya wanawake, kutelekeza na hata mauaji.

Tunashauri vyombo vya ufuatiliaji na usimamizi wa sheria na haki vizichukue na kuzifanyia kazi kwa ajili ya ustawi wa taifa letu ili tamasha liwe na tija.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Viongozi maadui uwekezaji hawafai

**KUWAPO** viongozi wanaojinufaisha na posho nono wanazojipangia kulipwa wanapokutana na kampuni zenye nia ya kuwekeza siyo tu kuwa wanaipaka Tanzania matope bali wanakwamisha juhudi za serikali kukuza uchumi.

Ni wahujumu wanaozima juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan, za kuinua uwekezaji na kufikia maendeleo kiuchumi.

Hivi karibuni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Dk. Binilith Mahenge, ananukuliwa akisema mwekezaji anaweza kwenda kwenye halmashauri yoyote kwa nia ya kuwekeza, lakini viongozi wakiwamo madiwani wanaweza kuwa kikwazo.

Dk. Mahenge anatoa mfano kuwa kuna mwekezaji alikwenda kwa nia ya kutaka kuwekeza kwenye eneo ambalo lilikuwa la serikali, lakini viongozi wakajipangia bajeti ya kulipana posho nyingi za kuandaa hati, mwekezaji akakata tamaa na kwenda kuwekeza nchi nyingine.

Mwenyekiti wa Bodi ya TIC, anasema tukio hilo ni miongoni mwa changamoto ambazo wawekezaji wa ndani na nje wamekuwa wakikumbana nazo wanapotaka kwenda kuwekeza kwenye halmashauri kutokana na uwekezaji kutotengewa maeneo.

Changamoto nyingine ni maeneo yanayotengwa wakati mwingine yanakuwa na migogoro ya mara kwa mara na hivyo kuwakatisha tamaa wawekezaji na kuamua kwenda kwenye mataifa mengine.

Serikali imekuwa na nia njema kwa halmashauri zote na imekuwa ikitenga maeneo ya uwekezaji kwani ni suala muhimu katika maendeleo ya nchi, kukuza uchumi wa taifa na wananchi wake.

Tunamshukuru Dk. Mahenge kwa kufichua viongozi wa aina hiyo kwani wameonyesha udhaifu mkubwa na ulafi, hivyo kukwamisha jitihada za kuvutia wawekezaji badala yake wamekuwa wakiwakatisha tamaa na kuwavuruga na mwisho kuondoka ili kuweka vitega uchumi mataifa yenye uwazi na ufanisi zaidi.

Viongozi hao wasivumiliwe hata kupewa dhamana kwani wanakuwa kikwazo kikubwa kwa serikali kuongeza vitega uchumi, mapato, ajira na kupunguza umaskini wa kipati kutokana na kukimbiwa na wawekezaji ambao wangelipa kodi kuajiri Watanzania na kuchangia maendeleo ya nchi.

Viongozi hao pia hawastahili kuitwa viongozi kwa sababu vitendo vyao hivyo vinakwamisha mpango wa taifa kuongeza fursa za kiuchumi, kijamii, kimaendeleo na kufikia uchumi wa viwanda.

Tumeshuhudia vijana wengi baada ya kuhitimu elimu ya vyuo vikuu ndani na nje ya nchi wamekuwa wakilalamikia serikali kwa kukosa ajira na kujikuta wakihaha kwa muda mrefu bila ya kuwa na kipato na baadhi yao kuamua kujiajiri wenyewe katika miradi ya ujasiriamali.

Uwekezaji wa kigeni ni njia mojawapo ya kukabiliana na tatizo hilo la ukosefu wa kazi kwa vijana, kwa vile nchi imeruhusu raia kutoka wa kigeni kuwekeza katika sekta mbalimbali ni jukumu la viongozi kushirikiana nao na kuwapa nafasi ya kukamilisha azma yao.

Viongozi wanaokwamisha vitega uchumi waache ukiritimba kwa kuendekeza kulipwa posho, waunge mkono jitihada za Rais Samia za kuifanya Tanzania kuwa ya uwekezaji kwani amekuwa akitumia ziara zake nje pamoja na kukaribisha na kuhamasisha wawekezaji.

Watanzania walio wengi wameshuhudia jinsi ziara zake hizo zilivyochukua jukumu hilo na zinavyoendelea kuleta tija na kwa taifa baada ya wawekezaji wengi kujitokeza na kuja kuwekeza.

Tatizo linalojitokeza sasa kuna baadhi ya viongozi hao wameonyesha zaidi kukwamisha uwekezaji kama ambavyo anaeleza Dk. Mahenge.

Inawezekana siyo tu mwekezaji huyo amekimbia nchini, huenda wapo wengi ambao walikutana na changamoto kama hiyo ya kuwekewa bajeti ya posho nyingi, lakini hawajajulikana.

Mungu ibariki Tanzania iondokane na viongozi hao wachache wasioitakia mema kwa kuendekeza ulafi wa fedha kwa manufaa yao binafsi huku wakiwaacha wanahitimu wa vyuo wakihaha mitaani iwe ni kutafuta kazi mwaka hadi mwaka bila mafanikio.

Lakini, kuikosesha nchi mapato ambayo yangetokana na kulipa kodi, kuuza bidhaa nje, kuingizwa teknolojia za kisasa na masoko kuuza bidhaa pamoja na huduma ambazo pamoja na kuuzwa nje nyingine zingebakia nyumbani.

## HABARI KITAIFA

# Zitto ataja mambo 15 yaliyokwaza upinzani uchaguzi mdogo Mtambwe

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimedai kuna watu katika serikali na Chama Cha Mapinduzi (CCM) hawataki kuheshimu kwa dhati misingi ya maridhiano yaliyofikiwa kati ya marehemu Maalim Seif Sharif Hamad na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, alitoa kauli hiyo jana katika ofisi kuu za chama zilizoko Vuga, Zanzibar alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu alichokiita vitimbi na hujuma zilizojitokeza katika uchaguzi mdogo wa Jimbo la Mtambwe, Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Hata hivyo, ACT-Wazalendo imetangazwa mshindi katika uchaguzi huo kupitia mgombea wake, Muhammed Ali Suleiman.

Zitto alidai chama chao katika uchaguzi huo kimeshuhudia mambo 15 ya hujuma na vitendo vinavyokwenda kinyume cha misingi ya haki za binadamu, demokrasia na utawala bora vilivyofanywa na askari wa vikosi vya serikali.

Alidai kuwa mgombea wa chama chao alitengenezewa njama za kubambikwa kitambulisho bandia ili aonekane ana vitambulisho viwili vya Mzanzibari Mkaazi.

Zitto alidai ni njama zilizoratibiwa wilayani Wete ili kumwondolea sifa za kuwa mgombea. Alikata rufani na kushinda.

Vilevile, alidai walibaini daftari la wapigakura lilikuwa na wapigakura wengi kuliko wapigakura halisi wa Jimbo la Mtambwe na walifanikiwa kupata vielelezo vya kura bandia ambazo zilizagaa katika vituo wakati ni kinyume cha sheria za uchaguzi.

Alidai baadhi ya maofisa wa serikali walikuwa wanatumia vibaya madaraka yao kuwabambika kesi watu waliokuwa wanahoji vitendo vya uvunjifu wa sheria vilivyokuwa vinajitokeza katika vituo vya kupiga kura.



"Wasimamizi wa uchaguzi waliwapata wapigakura ambao ni wana CCM kupiga kura zaidi ya moja na tukio hili lilikithiri katika Shule ya Uondwe na watendaji wa ZEC (Tume ya Uchaguzi Zanzibar) waliingia katika vituo wakiwa na kura mifukoni na kuziingiza kwa nguvu katika masanduku ya kura kinyume cha sheria," Zitto alidai.

Mwanasiasa huyo pia alidai baadhi ya wasimamizi waliziharibu kura kwa makusudi kwa kuzitia wino, kuzichora, kutogonga muhuri kwa zile karatasi ambazo mpigakura wake anaaminika kuwa ni wa ACT pamoja na mawakala kujitutumua kutetea sheria ndani ya vituo walitolewa nje na askari ili kuhakikisha CCM inapata uhuru wa kufanya wanavyotaka katika uchaguzi huo.

"Baadhi ya kura za mgombea wa ACT alipewa mgombea wa CCM wakati wa kuhesabu kama ilivyoshuhudiwa katika Shule ya Bwagamoyo na Uondwe katika jimbo hilo la Mtambwe na mawakala wetu walitolewa kwa nguvu na kupigwa na askari, jambo ambalo ni kinyume cha misingi ya haki za binadamu na utawala bora," alidai.

Zitto pia alidai kuwa katika uchaguzi huo kulikuwa na matumizi mabaya ya mali za serikali kama magari kufanya kazi kwa manufaa ya CCM.

"ACT tunaamini hakuna nia thabiti ya kusimamia mageuzi ya kisiasa ili kuwa na uchaguzi huru na wa haki, mambo yanayofanyika yamelenga kuwanufaisha watawala kuendelea kubakia madarakani lakini wanavunja misingi ya demokrasia, haki za binadamu na utawala bora," alidai.

Alisema wameamua kuweka hadharani hayo ili taasisi zote zinazosimamia haki za binadamu, utawala bora, asasi za kiraia na taasisi za dini kufahamu yanayoelezwa katika majukwaa na viongozi na hata katika nyumba za ibada juu ya ujenzi wa maridhiano na amani ya kudumu na Rais Dk. Mwinyi hajaonesha dhamira ya kufanya mageuzi yoyote ya maana ili kujenga misingi ya utawala bora.

Alisema kinachofanyika sasa, demokrasia na utawala wa sheria ambavyo ndiyo muhimili wa amani, umoja wa kitaifa na maridhiano katika nchi inaendelea kuvunjwa na uchaguzi wa mwaka 2025 wanaamini utakuwa na hujuma na uvunjifu wa haki za binadamu zaidi ya uchaguzi wa mwaka 2020.

Alisema ACT-Wazalendo wameandaa kongamano Desemba 8 siku ambayo Maalim Seif wakati wa uhai wake aliapishwa kuwa Makamu wa Rais. Watatoa tathmini na msimamo wa chama kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Akizungumzia uandikishwaji wa wapigakura utakaoanza Desemba mwaka huu, Zitto aliwataka wanachama wa ACT kujitokeza kwa wingi na chama kiko tayari kulinda haki za kidemokrasia ikiwamo ya kuchagua viongozi wanaowataka katika uchaguzi wa mwaka 2025.

Viongozi wengine waliohudhuria kwenye mkutano huo ni mwenyekiti wa chama hicho, Juma Duni Haji, Makamu Mwenyekiti ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman.

Hata hivyo, baada ya kutolewa malalamiko hayo ya ACT-Wazalendo siku ya uchaguzi huo, Mwenyekiti wa ZEC, Jaji Joseph Kazi alidai hajapelekewa rasmi ofisini madai hayo.

Mkurugenzi wa ZEC, Thabit Idarous Faina, akizungumza na Nipashe jana visiwani hapa, alisema tume inaongozwa kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Mwaka 2018 na wanasiasa wanazijua taratibu katika kushughulikia upungufu unaojitokeza na fursa ipo wazi kwa vyama kwa wanaohisi kuna tuhuma katika mchakato wa uchaguzi. Wanayo fursa ya kwenda mahakamani kupinga matokeo.

Alisema mahakama ndio muhimili utakaothibitisha tuhuma hizo kwa sababu ufanyaji kazi wa tume unazingatia sheria na kuna sehemu waliyokengeuka.

"Wanaposema kama kuna kura feki hilo ni kosa ambalo lilipaswa lishtakiwe katika vyombo husika ili haki itendeke kwa kosa hilo lilofanyika, kama waziona wamechukua hatua gani kisheria kwa sababu ili twende vizuri lazima twende na utawala unaofuata sheria ili tusiwe watu wa kuropoka na kusema vitu ambavyo havina ushahidi na kama unao ushahidi unajua utaratibu gani ufuate ili kupata haki," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema madai ya mgombea wao kuwekewa pingamizi, ni takwa la kisheria na kama kuna mtu anahisi kuna haja ya kutaka maelezo na kukata rufani na ndicho alichokifanya mgombea wao na tume ikajiridhisha kuwa hakuna ushahidi wenye kujitosheleza kuhusu madai ya kuwa na vitambulisho viwili vya Mzanzibari Mkaazi na tume ikatoa fursa kuwa wagombea.

Alisema vyama vya siasa vinapaswa kufuata sheria na jambo lolote ambalo wanahitaji maelezo dhidi ya tume, wafika tume kwa ajili ya kupata ufafanuzi na kama hawakuridhika, waende mahakamani.

Pia aliwataka wanasiasa kuendelea kuheshimu sheria ili kufanya mambo kwa kitaalamu na kuwaeleza wananchi jinsi gani siasa zinazohitajika kwa wakati huu na kipi wanachohitaji kwa sababu wananchi wanahitaji maendeleo na si siasa ambazo hazina mustakabali mwema kwa taifa.

# Imbeju yatoa mtaji wa mamilioni na bajaji kuwezesha wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuendeleza uwezeshaji wananchi, CRDB Bank Foundation kupitia Programu ya Imbeju, imetoa mtaji wa Sh. milioni 35 na bajaji moja yenye thamani ya Sh. milioni 10 kwa baadhi ya wanachama wa Taasisi ya Open Mind and Thoughts Organization (OMTO).

Wanufaika wa mtaji huo wezeshi ni miongoni mwa wanawake zaidi ya 110,000 waliopata mafunzo ya ujasiriamali yanayolenga kuwajengea uwezo wa kuendesha biashara kisasa kwa kuzingatia vigezo vya kimataifa.

Mtaji huo wezeshi umekabidhiwa na Mkuu wa Uendeshaji wa Taasisi ya CRDB Bank Foundation, Joycelean Makule kwenye mkutano mkuu wa tano wa mwaka wa OMTO uliofanyika jijini hapa.

Mkuu huyo aliyemwakilisha Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB Bank Foundation, TullyEsther Mwambapa aliwasisitiza wanachama wa OMTO kuutumia mtaji waliokabidhiwa kwa malengo yaliyokusudiwa ili warejeshe kwa wakati na fedha hizo ziwasaidie wengine.

"Mpaka sasa taasisi yetu ya CRDB Bank Foundation imeshakopesha zaidi ya Sh. bilioni 1.2 kati ya Sh. bilioni tano zilizotengwa kutekeleza Program yetu ya Imbeju.

"Ninawasihi ninyi mlionufaika mwanzoni mzitumie fedha hizi kwa umakini ili mzirejeshe ziwanufaishe wanachama wengine na wanawake wenzetu wenye uhitaji waliopo nchi nzima," alisema Joycelean.

Kuhusu bajaji aliyoikabidhi, alisema imekatiwa bima kubwa (comprehensive insurance) kumhakikishia mmiliki kinga dhidi ya majanga yanayoweza kujitokeza barabarani, nyumbani au popote atakapoiegesha.

Taasisi ya OMTO ina mtandao wa vikundi zaidi ya 200 nchini kote vinavyowajumuisha wanawake wanaopambana kuchangamkia fursa za ujasiriamali na inashirikiana na kila mdau mwenye nia ya kuwakomboa wanawake kiuchumi.

Mkurugenzi Mtendaji wa OMTO, Anna Haule, alisema tangu Programu ya Imbeju ilipozinduliwa Machi mwaka huu, walikuwa miongoni mwa watu wa mwanzo kuvutiwa na fursa zake na anayo furaha kuona malengo hayo yanaanza kutimia.

"Kuimarisha uchumi wa mwanamke ndio lengo letu namba moja. Tuliposikia Imbeju inawalenga wanawake hatukulaza damu, na leo (jana) kila mmoja hapa ni shahidi kwa macho yake.

"Wenzetu waliokidhi vigezo wamepewa mtaji wezeshi walioomba na wengine wanaendelea kukamilisha utaratibu ili wapewe mahitaji waliyoyaeleza. Ninaishukuru sana Benki ya CRDB hasa taasisi yake ya CRDB Bank Foundation kwa kutushika mkono," alisema Anna.

Mnamo Juni mwaka huu, ikiwa ni miezi mitatu tangu kuzinduliwa kwa CRDB Bank Foundation sambamba na programu yake ya Imbeju, waliingia makubaliano ya kushirikiana na OMTO ili kutoa elimu kwa wanawake na kuwawezesha kwa mtaji.

Programu ya Imbeju inayotoa mafunzo ya ujasiriamali, kukuza na kuendeleza biashara, na kutoa mtaji wezeshi kwa wanawake na vijana, inatekelezwa kupitia madirisha mawili.

La kwanza ni uwezeshaji wa vijana wenye ubunifu wanaoendesha kampuni changa (startups)linaloendeshwa kwa mfumo wa ushindani. Maombi huwasilishwa kupitia Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) au Tume ya TEHAMA (ICTC).

Dirisha la pili ni mahsusi kwa ajili ya wanawake na vijana wajasiriamali waliopo kwenye vikundi vilivyosajiliwa na ambavyo vimefanya kazi walau kwa miaka mitatu.

Vikundi hivi ni lazima viingie mkataba wa makubaliano na CRDB Bank Foundation kuruhusu wanachama wake kufaidika na mtaji wezeshi unaotolewa chini ya Program ya Imbeju.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Ukuta kujengwa fukwe za Bahari ya Hindi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

NAIBU Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, amesema serikali inatarajia kuanza tathmini ya ujenzi wa ukuta katika fukwe za Bahari ya Hindi na maeneo ya Nungwi, Mkoa wa Kaskazini, Zanzibar.

Amesema kwa kuwa fedha zimeshapatikana na andiko limewasilishwa kwa Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) kwa ajili ya michoro kuainisha aina ya ukuta unaotakiwa kujengwa.

Khamis aliyasema hayo bungeni jijini hapa jana alipojibu swali la Mbunge wa Nungwi, Simai Hassan Sadiki aliyetaka kujua ni lini tathmini ya ujenzi wa ukuta katika maeneo yaliyoathiriwa na bahari huko Nungwi itafanyika.

Naibu Waziri alifafanua kuwa kabla ya kujenga ukuta, serikali itafanya utafiti kujua ni aina gani ya ukuta unaofaa kujengwa katika eneo hilo ambao utasaidia kuzuia mawimbi yasifike kwenye makazi ya wananchi ili waendelee kufanya shughuli za kiuchumi.

Alisema serikali imechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali ya fukwe za Bahari ya Hindi.

"Kwa mwaka wa fedha 2023/24, serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar imetenga Sh. milioni 650 kwa ajili ya tathmini ya awali ili kufanya usanifu wa miundombinu itakayosaidia kurudisha fukwe katika hali yake," alisema Khams.

Ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, aliwahimiza wananchi wa maeneo ya Nungwi kuongeza jitihada za kupanda mikoko ambao inasaidia kupunguza mawimbi ya bahari katika fukwe na kutochimba mchanga kiholela.

Naibu Waziri Khamis pia aliwataka wananchi kuacha kutupa taka ovyo katika fukwe ili kulinda mazingira huku akitoa rai kuhamasisha kilimo cha mwani kisichoharibu fukwe.

"Ninapenda kuchukua nafasi kuhimiza uongozi na wananchi wa Nungwi kuongeza jitihada za kutunza mazingira ya maeneo ya ufukwe wa Nungwi kwa kudhibiti shughuli zisizo endelevu za kibinadamu kwa kuongeza jitihada za kuhifadhi mazingira na upandaji wa miti," alisema.

Aliongeza kuwa ili kutatua changamoto ya shughuli za uvuvi usiozingatia, hifadhi ya mazingira na matumizi ya fukwe yasiyo endelevu, serikali imechukua hatua mbalimbali ikiwamo kutoa elimu kwa wavuvi na wananchi kwa ujumla wajikite katika uvuvi rafiki kwa mazingira.

Khamis pia alisema serikali kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali inafanya doria katika maeneo ya bahari na kuchukua hatua za kuangamiza nyavu zinazotumika katika uvuvi haramu kwa lengo la kuhifadhi mazingira ya bahari.



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (katikati), akimsikiliza Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ughani wa Uvuvi, Anthony Dadu (kulia), wakati akielezea matumizi ya baadhi ya vifaa vya uvuvi wa kisasa baada ya waziri kukabidhi boti 14 za kisasa kwa wavuvi mkoani Tanga zenye thamani ya Sh. bilioni 1.2 kwa kushirikiana na Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB). Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Waziri Kindamba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ujira wa wapagazi na wapishi KINAPA waibua jambo bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeliarifu Bunge kuwa inatarajia kufanya kikao kazi cha wapagazi, wapishi na waongoza watalii Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro (KINAPA) na waajiri wao ili kupendekeza viwango vya malipo ya ujira na kuwasilishwa katika Bodi ya Utatu.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula, alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Vunjo (CCM), Dk. Charles Kimei aliyetaka kujua lini serikali itafanya mapitio ya viwango vya malipo ya ujira kwa wapagazi, wapishi na waongoza watalii katika hifadhi hiyo.

Akijibu swali hilo, Kitandula alisema bodi hiyo ndio yenye dhamana ya kumshauri waziri mwenye dhamana ili makubaliano hayo yawe ya kisheria.

"Serikali inatambua changamoto ya viwango vya malipo ya ujira kwa wapagazi, wapishi na waongoza watalii katika Hifadhi ya Taifa Kilimanjaro.

"Katika kutatua changamoto hizo, wizara kwa kushirikiana na vyama vya mawakala wa utalii, yaani waajiri, imeanza kutekeleza mikakati mbalimbali kwa ajili ya kufanya maboresho ya viwango hivyo vya malipo ya ujira," alisema.

Kufuatia hatua hiyo, alisema wizara imefanya kikao na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kujadili kuhusu viwango vya ujira kwa wapagazi, wapishi na waongoza watalii.

"Hatua inayofuata ni wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kufanya kikao kazi baina ya wadau hao na waajiri wao kwa lengo la kupendekeza viwango stahiki ili viweze kuwasilishwa katika Bodi ya Utatu yenye dhamana ya kumshauri waziri mwenye dhamana ili makubaliano hayo yawe ya kisheria.

"Kikao hicho kinatarajiwa kufanyika katikati ya Novemba mwaka huu jijini Arusha," alibainisha.

# TAKUKURU yachunguza ujenzi wa kituo cha afya

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga imeanza uchunguzi wa awali katika mradi wa ujenzi wa Kituo cha Afya Bulige, Halmashauri ya Msalala wilayani Kahama wenye thamani ya Sh. milioni 630 kutokana na kudaiwa kujengwa chini ya kiwango.

Mradi huo ambao haujakamilika, unadaiwa kuwa na kasoro mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi wake kuwa chini ya kiwango.

Hayo yalibainishwa jana na Kaimu Kamanda wa TUKUKURU Mkoa wa Shinyanga, Mwamba Masanja, alipotoa taarifa kwa vyombo vya habari kuhusu utekelezaji wa majukumu yao kwa kipindi cha miezi mtatu ya Julai hadi Septemba mwaka huu.

Alisema taasisi hiyo ilifanya ufuatiliaji wa miradi miwili; ujenzi wa Kituo cha Afya Bulige na ujenzi wa Shule mpya ya Msingi Maganzo wilayani Kishapu. Ilibaini upungufu katika miradi hiyo huku Kituo cha Afya Bulige wakianza uchunguzi wa awali.

Alisema katika ujenzi wa Shule mpya ya Msingi Maganzo chini ya mradi wa Boost wenye thamani ya Sh. milioni 561.1, walibaini upangufu katika jengo la utawala kutowekwa vigae, mikanda ya gypsum kubanduka, dari kuanza kutoa nyufa na kutoa ushauri kurekebishwa kwa upungufu huo haraka.

Vilevile, alisema walifanya uchambuzi katika mfumo wa Kodi ya Zuio katika ununuzi wa vifaa na utoaji huduma kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kubaini kwamba katika mwaka wa fedha 2022/23, jumla ya Sh. milioni 83.3 ikiwa ni fedha za Kodi ya Zuio zilizokatwa na wazabuni na watoa huduma hazikuwasilishwa TRA kama sheria inavyosema.

Alisema kuwa kwa kipindi hicho walifungua kesi tatu mahakamani, huku kesi tano za uhujumu uchumi zikiamuliwa na washtakiwa wote walikutwa na hatia na kuhukumiwa.

Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Shiyanga alisema wana kesi nyingine tisa za makosa mbalimbali zinaendelea mahakamani.

Alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, kuendelea kutoa taarifa pale wanapoona viashiria vya vitendo vya rushwa ikiwamo katika miradi ya maendeleo.

Alifafanua kuwa wananchi wanapoona viashiria hivyo, wafike katika ofisi za TAKUKURU au kupiga simu bure kwa namba 0738150196 ili wafanyie kazi na kuzuia vitendo hivyo kwa maendeleo ya nchi.

## Watu 320 kushiriki 'Twenzetu Kileleni'

**Na Mary Mosha,** MOSHI

WAZALENDO 320 wanaoshiriki Kampeni ya 'Twenzetu Kileleni' inayoongozwa na Jenerali mstaafu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), George Waitara, kwa ajili ya kupandisha bendera ya taifa katika kilele cha Uhuru cha Mlima Kilimanjaro, wamepanga kuanza safari hiyo Desemba 3, mwaka huu.

Kampeni hiyo itanogeshwa na ndege maalum ya uokozi na timu ya madaktari watakaotoa huduma mbalimbali za afya kwa washiriki hao watakaohitimisha safari yao Desemba 9 siku ya Uhuru wa Tanganyika.

Akizindua kampeni hiyo jana, Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Nurdin Babu, alisema kampeni hiyo ni sehemu ya kuhakikisha utalii unaongezeka katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA) na kukuza mapato ya nchi kwa ujumla.

"Tumedhamiria kuhakikisha utalii katika Hifadhi ya Taifa ya Kilimanjaro unakimbia, huduma za kiusalama zipo vizuri na ndege za uokoaji kwa watalii wa ndani na nje. Tuna timu za wataalamu wa kitabibu watakaotoa huduma mbalimbali, hii yote ni kuhakikisha watakaopanda mlima, wanafika salama bila tatizo lolote. Watanzania msiogope jitokezeni kwa wingi," alisema.

Kwa mwaka huu, Kampeni ya Twenzetu Kileleni, imeongezewa wigo baada ya waandaaji kuongeza idadi ya malango yatakayotumika kufikia matatu. Malango hayo ni Machame (Hai), Marangu (Moshi) na Lemosho (Siha).

Awali, Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi wa KINAPA, Glady Ng'umbi, alisema kuongezwa kwa njia zitakazotumika, kutasaidia Watanzania wengi kujionea vivutio mbalimbali zilivyopo katika hifadhi hiyo na kuwa mabalozi wazuri wa uhamasishaji.

"Kampuni ya Uwakala wa Utalii zinazotarajiwa kupandisha wazalendo hao ni pamoja African Scenic Safari, ZARA Tanzania Advantures na African Zoom. Tumejipanga vizuri katika uhamasishaji wa utunzaji wa mazingira, ila kabla ya hapo tutafanya kampeni maalumu ya ufanyaji wa usafi katika eneo la hifadhi," alisisitiza.

Mkurugenzi wa ZARA Tanzania Advantures, Zainabu Ansell, aliwataka Watanzania kujitokeza kufanya utalii katika hifadhi hiyo ya Taifa ya Kilimanjaro, kuona matunda ya uhifadhi na namna unavyotoa fursa ya kuongeza ajira na pato la taifa.

Kabla ya uzinduzi huo, Katibu Tawala wa Mkoa Kilimanjaro (RAS), Tixon Nzunda, alisema ikiwa Watanzania watajitokeza kwa wingi kutembelea vivutio vya utalii kutasaidia ukuzaji wa uchumi na uendelezaji wa miradi.

# Kampuni zapigwa 'stop' uuzaji wa viwanja

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imetangaza kibano dhidi ya kampuni binafsi zinazojihusisha na biashara ya kuuza viwanja vya makazi na biashara katika Jiji la Arusha, baada ya kuzipiga 'stop' kufanya kazi hiyo.

Aidha, imeagiza idara ya ardhi na mipango miji jijini humo, kusimamia kikamilifu uuzaji wa viwanja hivyo katika maeneo yote, kwa ajili ya kulipanga jiji hilo la kitalii.

Zuio dhidi ya kampuni hizo, limetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa.

Kuhusu kampuni binafsi zinazofanya biashara ya kuuza viwanja katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, Mtahengerwa alisema: "Kuanzia sasa ni marufuku kufanya biashara hiyo hapa, kwa sababu zinachangia kwa kiasi kikubwa Jiji kutopangwa vizuri.

"Hii idara ya ardhi na mipango miji, ina wasomi wa kutosha na wenye weledi wa kutosha. Simamieni mpango huu, tumieni taaluma zenu kuupanga mji wa Arusha ambao ni jiji la kitalii.

"Msiache kampuni binafsi zitupangie mji wetu. Ukipita kila mahali unakuta matangazo ya kampuni binafsi zinauza viwanja, ukiangalia ni viwanja vya 10 kwa 10. Ni nani atakuja kurekebisha hayo makosa kama siyo sisi?"

Aidha, Mtahengerwa alisema kuna baadhi ya watumishi wa umma katika jiji hilo wanahujumu mapato ya serikali kwa maslahi yao binafsi.

**Zuio dhidi ya kampuni hizo, limetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa.**

Meya wa Jiji la Arusha, Maximilian Iraghe, alisema katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2023/24, serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni tatu kutoka kwenye mapato yake ya ndani ya kuzielekeza kwenye miradi mbalimbali ya maendeleo katika halmashauri hiyo.

Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Juma Hamsini, alisema katika kuimarisha ulinzi katika Jiji hilo wameshafunga kamera za barabani 10 na kwamba lengo ni kufunga kamera 100 ili kudhibiti vitendo vya uhalifu.



Katibu Mwenezi wa CCM Mkoa wa Manyara, John Thobias Nzwalile (kushoto), akikaribishwa na Katibu wa CCM Manyara, Iddi Mkowa, baada ya kuwasili kwenye kituo chake cha kazi Mjini Babati juzi, kulia ni Katibu wa Jumuiya ya Wazazi, Christina Masagasi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Manyara yatishiwa ongezeko watoto wenye tatizo la usikivu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKOA wa Manyara, unatishiwa na ongezeko jipya la watoto wenye tatizo la usikivu na magonjwa ya sikio, kutokana na masikio yao kugundulika kuathiriwa na matumizi ya pamba masikioni, mafua na kelele za muziki.

Hospitali ya Rufani ya Mkoa huo, kwa wiki moja, inapokea kati ya watoto 10 mpaka 20, wenye umri chini ya miaka mitano wenye tatizo la masikio.

Katika mahojiano maalum na Nipashe jana, Daktari Bingwa wa Masikio, Pua na Koo wa hospitali hiyo, Athanas Budodi, alisema athari kubwa zimegundulika kutokea katika sikio la nje, sikio la kati na la ndani.

"Ugonjwa wa masikio, unasababishwa na vitu vingi. Unaweza kuupata kutoka magonjwa ya kuzaliwa, kuambukiza, ajali, mifumo ya fahamu na mengine husababishwa na baadhi ya dawa zinazoleta sumu na kuharibu mfumo wa masikio.

"Vilevile, shida ya masikio kwa watoto chanzo ni kurithi kutoka kwa wazazi, wakati wa ujauzito kama mama haudhurii kliniki vizuri, mtoto anaweza akapata shida ya masikio kutokana na virusi vya rubella na kaswende. Mtoto akiwa tumboni anaweza kuharibika masikio au akazaliwa na tatizo la masikio na likamtesa," alisema Dk. Budodi.

Alitaja chanzo kingine ni magonjwa ya kuambukiza kama fangasi, huku akisisitiza wazazi kutumia pamba kusafisha masikio kuna haribu sikio la nje.

Aidha, alisema mtoto anapougua mafua yuko kwenye hatari ya kupata shida ya masikio, maana wadudu wanaweza kutoka kwenye pua wakaingia sikio la kati.

"Pia kuna sauti au kelele, nazo ni chanzo cha masikio kuharibika na mtoto akipigwa kibao au kofi vinasababisha sikio la mtoto kuharibika," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Budodi, kipindi cha mvua za masika idadi ya watoto wanaougua masikio, huongezeka zaidi kwa kuwa wengine wanaweka maharage kwenye sikio na wengine huweka mbaazi, karanga na mazao mengine.





# Jeshi la Zimamoto lataka ushirikiano kukabili majanga

**Na Remmy Moka,**
SAUT

JESHI la Zimamoto na Uokoaji mkoani Mwanza limewaomba wananchi kutoa ushirikiano katika kukabiliana na majanga mbalimbali yakiwamo ya moto kwenye maeneo mbalimbali.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza, Mrakibu wa Zimamoto (SF) Kamila Labani, alisema hayo jana wakati wa kufunga mafunzo ya utayari ya jeshi hilo yaliyoendeshwa na wakufunzi kutoka Umoja wa Mataifa (UN).

Lengo la mafunzo hayo ni kuimarisha usalama katika kiwanja cha ndege mkoani hapa.

Alisema jeshi hilo linategemea zaidi taarifa kutoka kwa wananchi pindi yanapotokea majanga ili kufika katika maeneo husika kwa wakati kabla hayajasababisha madhara makubwa.

Vilevile alisema katika mafunzo hayo yaliyofanyika kwa siku nne yakishirikisha zaidi ya askari 60 kutoka wilaya zote za mkoa wa Mwanza pamoja na uwanja wa ndege wa Mwanza yalilenga kuwapa ufahamu wa fizikia ya moto pamoja na namna nzuri ya kuokoa maisha na mali za watu katika majanga ya moto.

Labani alisema taarifa iliyotolewa na Shirika la Anga Duniani (ICAO) ilibainisha takwimu za hivi karibu kuwa Tanzania ni nchi ya nne kwa usalama wa anga barani Afrika, hivyo wanajitahidi kudhihirisha umahiri wa jeshi hilo kikosi cha Zimamoto na Uokoaji katika maeneo hayo.

Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe, Hassan Bomboko, aliyemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amosi Makalla, katika kufunga mafunzo hayo, aliwatoa hofu wananchi na kuwataka kutoa taarifa mapema za majanga ya moto ili kuleta tija ya uokoaji.

**Alisema jeshi hilo linategemea zaidi taarifa kutoka kwa wananchi pindi yanapotokea majanga ili kufika katika maeneo husika kwa wakati kabla hayajasababisha madhara makubwa.**

Meneja wa Uwanja wa Ndege wa Mwanza, Musa Mchora, alisema katika miongozo ya Umoja wa Mataifa ni lazima kila kiwanja cha ndege kiwe na kikosi mahiri cha zimamoto na uokoaji kwa ajili ya usalama wa ndege, abiria na mizigo yao.

Pia alisema mafunzo hayo yamewaongezea ufanisi wa kazi askari wa kikosi hicho na pia wameongezewa ujuzi juu ya namna gani wanaweza kupambana na moto, kufanya uokozi wa waathirika wa moto katika jamii.



Ofisa wa Idara ya Tathmini na Ufuatiliaji wa Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Hans Obote (kulia), akiwaonyesha wadau wa kupinga ukatili, vitendea kazi ambavyo shirika hilo linatumia kutoa elimu dhidi ya rushwa, kwenye kikao kilichofanyika Makumbusho jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Maeneo korofi yaishtua TARURA

**Na Neema Sawaka,**
KAHAMA

WAKALA wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Kahama mkoani Shinyanga, imeanza mikakati ya kukabiliana na madhara ya mvua za El-Nino kwa kuunda kamati itakayobaini na kushughulikia maeneo korofi yanayoweza kuhatarisha watumiaji wa barabara kipindi cha mvua.

Meneja wa TARURA Wilaya hiyo, Mhandisi Job Mutagwaba, alisema hayo juzi alipokuwa akikagua barabara mbalimbali wilayani hapa na kuwataka wananchi kulinda mitaro dhidi ya taka ngumu ili isizibe na kusababisha mkusanyiko wa maji kwenye makazi.

Mhandisi Mutagwaba alisema Manispaa ya Kahama ina mtandao wa barabara kilomita 923.4 zikiwamo kilomita 11.72 kiwango cha lami, 110.5 kiwango cha changarawe na 8,01.5 kiwango cha udongo.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Mutagwaba alisema TARURA imeanza ukarabati wa baadhi ya barabara kukabiliana na mvua zinazonyesha.

"Eneo la kipande cha barabara itokayo mtaa wa Chesi kupitia Lyazungu hadi Maji Hoteli lenye urefu wa kilomita 4.9 limeanza kuboreshwa kwa kuwekwa changarawe kwa kuwa msimu wa mvua lilikuwa halipitiki kirahisi kwa kujaa maji," alisema.

Mhandisi Mutagwaba alisema maeneo korofi mengine ni Mhongolo, Kitwana, Nyasubi na Majengo ambayo mitaro iliyopo tayari imezibuliwa ili kuweza kupitisha maji na kuondoa kero kwa wananchi.

"Kwa mwaka wa fedha 2023/24 bajeti iliyokuwa imetengwa kwa fedha za mfuko wa barabara ni zaidi ya Sh. bilioni 1.18, mfuko wa jimbo Sh. milioni 500 na fedha za tozo Sh. bilioni moja. Kwa mwaka matengenezo ya barabara ni kilomita 82.91 sawa na asilimia 8.98," alisema.

Mwakilishi wa kampuni ya Arjaz Women Technology, Arafa Kisasi, iliyopewa zabuni ya matengenezo ya barabara ya kutoka Mtaa wa Chesi kupitia Lyazungu hadi Maji Hotel, alisema mkataba wake ni wa miezi minne kuanzia Septemba hadi Januari, mwakani.

Mmoja wa wananchi wa Mtaa wa Lyazungu, Happy Albert, alisema kipindi cha mvua maji yamekuwa yakiingia ndani ya nyumba, wanafunzi wanashindwa kuvuka na mifugo kusombwa na maji, hivyo kuiomba serikali kuhakikisha matengenezo hayo yanakamilika mapema kabla ya mvua hazijasababisha madhara.

# Wajasiriamali waomba kutumia vyoo vya shule

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAJASIRIAMALI wa gulio lililoko jirani na Shule ya Msingi Nyahanga katika Manispaa ya Kahama, wamemwomba Mkurugenzi wa Halmashauri kuwabadilishia siku ya gulio kuwa Jumatatu tofauti na ilivyokuwa Jumamosi ili watumie vyoo vya shule.

Eneo hilo liko katikati ya shule za msingi Nyahanga"A" na "B" pamoja na barabara kuu ya kwenda nchi jirani za Rwanda, Burundi, Uganda na Jamhuri ya Kimokrasia ya Congo (DRC) na wateja wao ni wakazi wa kata hiyo na watumiaji wa barabara hiyo.

Ombi lao kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, linakuja kutokana na gulio hilo kutokuwa na huduma ya choo hali inayosababisha wafanyabiashara na wajasiriamali hao kujisaidia ovyo na kuhatarisha afya zao pamoja na wanafunzi wa shule hizo.

Mmoja wa wajasiriamali hao, Juma Kulwa, alisema ombi lao la kufanya biashara Jumatatu litawasaidia kutumia vyoo vya shuleni hapo kwa kuwa Jumamosi vyoo hivyo vinakuwa vimefungwa na kuwafanya wakose sehemu ya kujihifadhi.

Naye Suzana Bundala alisema walikuwa wakifanya shughuli zao katika eneo hilo Jumatatu lakini Mkurugenzi akaamuru waanze kufanya siku za Jumamosi na kusema siku hiyo inakuwa na minada mingi na kuhofia kutokupata wateja kwa kuwa wanakuwa wametawanyika katika minada mingine.

Diwani wa Nyahanga, Pancras Ikongoli, alisema wajasiriamali hao hawakutakiwa kuwapo katika eneo hilo kwa sababu ni karibu na mazingira ya shule, hivyo wanaweza kuwasababishia usumbufu wanafunzi katika masomo yao.

Alisema, walijadili na kukubaliana na mkurugenzi kuwaruhusu kufanya biashara zao siku za Jumamosi ambayo wanafunzi wanakuwa nyumbani badala ya siku za masomo, hivyo kuwataka kuwa wavumilivu wakati wanashughulikia suala la vyoo katika eneo hilo.

Mkurugenzi wa Manispaa, Msumba, alisema eneo hilo halipaswi kuwa na gulio au mnada na kwamba kama haiwezekani kupatumia siku za Jumamosi basi watafute magulio mengine kwa kuwa katika manispaa hiyo, yako magulio mengi.

"Wanaweza kwenda huko na kufanya biashara zao bila kuvutana na mamlaka husika na minada mingi hufanyika siku za Jumamosi na Jumapili kuliko kusababisha usumbufu kwa wanafunzi," alisema Msumba.

**Ombi lao kwa Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Anderson Msumba, linakuja kutokana na gulio hilo kutokuwa na huduma ya choo hali inayosababisha wafanyabiashara na wajasiriamali hao kujisaidia ovyo na kuhatarisha afya zao**



Ukurasa 12

Ndivyo kisiwa hiki kinavyoelekea kuwa kitovu cha elimu bora



Ukurasa 13

Miaka 30 TGNP, ilivyojenga vuguvugu mabadiliko ya usawa wa kijinsia



Ukurasa 14

**Ujio mkataba wa plastiki hili ni angalizo kwa Afrika**


Nipashe

# TESA

Jumanne Novemba 7, 2023

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI


ELIMU

NA JULIETH MKIRERI, KISARAWE

KUZUIA WASICHANA KUKIMBIA SAYANSI...

# Shule inavyotumia wahadhiri vyuo vikuu 'kuwakochi', kupenda tahasusi

KAMPENI ya "Tokomeza Zero," inayoasisiwa na Katibu Mkuu wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Jokate Mwegelo, anaanzisha sekondari ya wasichana wilayani Kisarawe mkoa wa Pwani, inayolenga kulipa taifa wanasayansi mahiri.

Lakini, zimwi la kuogopa sayansi linaweza kuwakwamisha wasichana hao ambao wanakimbilia kwenye tahasusi za sanaa na kukwamisha lengo.

Sekondari hiyo iliyoanzishwa mwaka 2020 ikichukua wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha sita, inafanya kila mbinu ikiwamo kutumia wasomi vyuo vikuu kufunda mabinti kupenda sayansi.

Nipashe inakutana na Mkuu wa Shule Mariam Mpunga, anayeelezea kuwa katika shule hiyo mbinu zinazotumika ili wanafunzi wa kike wamudu masomo ya sayansi ni motomoto ikiwamo kutumia wasomi wa vyuo vikuu kuongeza hamasisha.

Anakumbusha kuwa mwaka 2020 Sekondari ya Jokate Mwegelo ilianza kuchukua wanafunzi 80 wa kidato cha tano wote wakisoma tahasusi ya sayansi.

Anaeleza kuwa japo juhudi kubwa zinafanyika wapo wasichana wanaofaulu masomo ya sayansi na baadaye kuyakimbia na kujiunga kozi za sanaa wakihofia ugumu wa kufaulu.

"Wanawake wanasayansi ni wachache ukilinganisha na wanaume, tunataka tupate wahandisi, madaktari na wataalamu wengine wengi wa sayansi. Sasa tukiendelea kuwaruhusu wasichana kubadili tahasusi za sayansi kwenda sanaa hatutafanikiwa," anasema.

Anaeleza kwamba wengi wa wasichana wamekuwa wakiogopa masomo ya sayansi kwa kuwa yanachukua muda mwingi kusoma na kujifunza mara kwa mara jambo wanalodai ni gumu.

Kwa mujibu wa Mariam ili kupata wanasayansi wanawake mahiri na maarufu baadaye, amebuni mbinu ya kukaribisha wahadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kukutana na wanafunzi hao na kuwapiga shule.

Anasema wahadhiri hao wamekuwa wakifika shuleni na kuwashawishi wanafunzi kusoma sayansi kwa bidii na kuwapa mbinu za kufaulu lengo kubwa likiwa ni kuwaondoa kwenye mawazo ya kubadilisha tahasusi.

"Ninawaleta madaktari wanawake pia ili watoe ushuhuda kwa hawa wanafunzi kwa pamoja tufanikiwe kumnyanyua mtoto wa kike afanye vizuri kwenye masomo ya sayansi," anasema Mwalimu Mariam.

Anasema mbali ya mbinu hiyo anawasilisha ombi lake kwa serikali kuwaandaa wanafunzi wakiwa shule za msingi kusoma zaidi sayansi hasa wasichana ili kurahisisha kazi ya kuwafunza na kuwahamasisha.

Anaeleza kuwa endapo kutakuwa na utaratibu huo na kuwaweka pamoja wanaoonyesha mwelekeo katika masomo hayo wakifika elimu ya sekondari inakuwa rahisi kwao kusoma na



Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Kisarawe, Mariam Mpunga. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

kufanya vizuri.

"Tupo walimu na serikali, kwa upande wa wazazi na walezi nao wana nafasi nzuri ya kuzungumza na watoto wao kuwashauri pamoja na kuwapa moyo. Ili wasikubali mtoto aliyefanya vizuri kwenye masomo ya sayansi abadilishe tahasusi aliyochaguliwa kwa kuhofia mambo yatakuwa magumu baadaye," anaonya.

"Niliahidi kusimamia watoto wa kike kwa karibu na nitaendelea kufanya hivyo shule yangu iongoze itoe wanafunzi bora wa masomo ya sayansi ambao watakuwa kielelezo kwa wengine baadaye," anasisitiza Mkuu wa Shule.

Anabainisha kwamba pamoja na shule hiyo kuanzishwa katika kampeni ya kutokomeza zero, kwasasa mambo yamebadilika na kampeni imekuwa ni kutokomeza daraja la tatu kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita, akimiani kuwa kwa ushirikiano na walimu na wazazi watafanikiwa.

Anasema shule hiyo ina wanafunzi zaidi ya 800 na uhitaji wa maabara pamoja na vifaa vyake ili kuwawezesha kufanya vizuri kwa kusoma kwa njia ya vitendo na majaribio.

Anawaomba wadau mbalimbali kujitokeza kusaidia kutatua kikwazo hicho hususani kufanikisha ujenzi wa maabara ya fizikia pamoja na mtaalamu wa maabara hatua ambayo itawafanikisha wanafunzi kufanya maandalizi bora kwenye mitihani ya shuleni na ya kitaifa.

Mwalimu Mariam anataja kukosa uzio akisema unahitajika kutokana na mazingira yake yalivyo ili kuimarisha ulinzi kwa wanafunzi na kuwaepusha na mambo hatarishi.

Kadhalika anaiomba jamii inayozunguka shule kuimarisha ulinzi kwa wanafunzi hao wa kike na kuishukuru serikali kwa kutoa fedha ambazo amezipokea kwa ajili ya ujenzi wa mabweni sambamba na vyumba vya madarasa na kuondoa vikwazo vilivyokuwapo awali.

"Mwaka huu nimepangiwa wanafunzi wa kidato cha tano 474 tofauti na mwaka jana ambapo nilipokea 70 pekee, hii ilinipa hofu kutokana na majengo niliyokuwa nayo lakini serikali imeliona hilo na kunipatia fedha za mabweni manne, vyoo matundu 18 pamoja na vyumba vya madarasa tatizo kwasasa hakuna," anasema Mkuu wa Shule.

INAENDELEA UK.14

ELIMU

NA NEEMA EMMANUEL, UKEREWE

# Ndivyo kisiwa hiki kinavyoelekea kuwa kitovu cha elimu bora

HAKIKA elimu ni ufunguo wa maisha kama wasemavyo wahenga lakini, mazingira ya kuifikia na kuipata ni jambo jingine. Ni kwa sababu itakupasa utembee kilometa nyingi kuifikia shule na kurudi nyumbani, uingie majini kwa kutumia mitumbwi kama unaishi visiwani na wakati mwingine uwe mtoro kukwepa usumbufu wa kuipata elimu.

Lakini hakuna marefu yasiyo na ncha, wilaya ya Ukerewe iliyoko mkoa wa Mwanza ilipitia mambo hayo, licha ya kukumbana na matumizi ya mitumbwi, kutembea umbali mrefu, utoro, mimba za utotoni, kukatisha masomo kwa sababu mbalimbali na ajali za majini zilizokuwa zikiwapata mara kwa mara katika safari ya kutafuta elimu, historia imebadilika.

Hayo yamekwisha ni baada ya zaidi ya billion 7.6 kuangukia kwenye sekta ya elimu sekondari na nyingine takriban bilioni 3.5 zikielekezwa msingi, si haba.

Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Ukerewe, Emmanuel Sherembi, anazungumza na Nipashe, akieleza kuwa katika sekta ya elimu wamepunguza adha walizokuwa wanazipata wanafunzi hasa kuvuka maji na mitumbwi na mara nyingi walikatisha masomo wanapata ajali.

Aidha, juhudi zimefanyika kuondoa msongamano madarasani kutoka wanafunzi 120 hadi 45 kwa darasa, yote yakiwapa hali bora walimu na wanafunzi na mchakato mzima wa kujifunza na kufunzwa.

Anasema ili kuweka mambo sawa wametekeleza miradi mbalimbali ikiwamo kapu la mama, fedha za UVIKO-19 na mradi wa boost ambayo kwa mwaka 2022 hadi 2023 vyumba vya madarasa 50 vimejengwa na 44 vya elimu msingi na sita ya awali vya mfano, huku matundu ya vyoo 64 yakijengwa, 48 vyoo vya msingi na 18 vya elimu ya awali.

"Kupitia mradi wa boost tumejenga matundu manne ya vyoo vya walimu, majengo mawili ya utawala yenye ofisi 10, nyumba moja ya walimu inayoweza kuishi familia zaidi ya moja, vichomea taka viwili, kutengeneza madawati 660 ya wanafunzi wa msingi na viti 90 na meza 90 za wanafunzi wa elimu ya awali,viti 50 na meza 50 za shule zote zilizotekeleza mradi pamoja na bembea 12 na viwanja kwa ajili ya wanafunzi wa elimu ya awali. " anaeleza.




Moja ya majengo ya kutoa huduma za elimu kisiwani Ukerewe. **PICHA: NEEMA EMMANUEL**

> Juhudi zimefanyika kuondoa msongamano madarasani kutoka wanafunzi 120 hadi 45 kwa darasa, yote yakiwapa hali bora walimu na wanafunzi na mchakato mzima wa kujifunza na kufunzwa.

Anaongeza kuwa pamoja na kutekeleza miradi yote kwa ubora unaotakiwa na kukamilika katika mradi wa boost Shilingi milioni 70 zimebakia na wanatarajia kuziombea kibali kuzitumia kuboresha miundombinu katika maeneo hayo ya miradi.

"Tunamshukuru sana Rais Samia Suluhu Hassan, kwa kutuangazia Ukerewe ..."anaeleza Sherembi.

### HALI ILIVYOKUWA

Mkuu wa Wilaya, Hassan Bomboko, anakumbushia tatizo lililvyokuwa, akieleza kuwa Ukerewe ni visiwa hivyo watoto walilazimika kwenda umbali mrefu kwa kutumia majahazi, boti na mitumbwi jambo lililofanyika kila siku, mwezi na mwaka wakisafiri kwa muda usiopungua saa mbili hadi tatu jambo lililochangia kusoma kwa shida.

Anaeleza kuwa serikali imejenga madarasa na mabweni kwa wenye uhitaji hivyo kwa kiasi kikubwa yatawahifadhi watoto hao na kuwaepusha na vishawishi kwani miaka ya nyuma wanafunzi wanaanza darasa la kwanza 40 na wanaomaliza ni 20.

"Kuna kisiwa kinaitwa Bwiru walikuwa na mtumbwi wao MV Tabutupu watoto walikuwa wanalazimika kuupanda kuja upande wa pili kufuata elimu sasa wanaondokana na adha hiyo, tunatoa elimu kwa jamii kumpa fursa mtoto hasa wa kike kusoma kwa sababu ndiye anayebeba taifa lazima tuwajengee uwezo," anaeleza Bomboko.

Anaeleza kuwa wanawapeleka walimu maeneo ya kisiwani kuwaimarishia miundombinu ili waweze kutoa elimu iliyobora pasipo kuwa na vikwazo na kuongeza uelewa na ufaulu kwa watoto hao.

### SAUTI ZA WADAU

Akizungumza na Nipashe Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Nakasahenge, Jenifer Damian, anasema katika Kata ya Namagondo anapofanyakazi zaidi ya watoto 300 wanatembea kilometa tano kufuata elimu.

Anaongeza kuwa kukamilika kwa Shule ya Msingi Kilimabuye, katika kata hiyo kutawanusuru watoto hao kutembea umbali mrefu ambao ulichangia kuwarudisha nyuma kitaaluma na hata wengine kuacha shule.

"Huku tunavipindi viwili vya masomo asubuhi na mchana ikifika saa 6:30 wanakwenda kupata chakula nyumbani na wanapaswa kurejea na vipindi vinaanza saa 8:00 lakini mara nyingi kipindi kimoja ama viwili wanavikosa kwa sababu ya umbali," anaeleza Jenifer.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Mulezi Charles Simeo, anaeleza kuwa matarajio ya shule kwenye miradi hiyo ni kupunguza msongamano madarasani awali wanafunzi zaidi ya 100 walikuwa wanatumia chumba kimoja hivyo wanaamini tatizo hilo litaisha na kupelekea kuinua kiwango cha taaluma kwa shule, wilaya, mkoa na kitaifa.

Aidha, Teopista Masalaji, mkazi wa Namagondo anaeleza kuwa watoto wao walikuwa hawamalizi masomo lakini sasa wameondokana na tatizo hilo pia mradi wa Boost waliupokea na wakashiriki ipasavyo hadi kuukamilisha.

Diwani wa Kata ya Namagondo, Thomas Ng'afu, anaeleza kuwa mradi huo ni ukombozi kwa watoto wao na itasaidia kupunguza wimbi la utoro na wanachosubiria ni kupata matokeo chanya kwa sababu shule itakuwa karibu hivyo wazazi na walezi watambue umuhimu wa elimu na kuwapeleka watoto shule.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya Ukerewe, Ally Mambile, anaeleza kuwa Rais ametoa fedha nyingi katika halmashauri hiyo kwa ajili ya miradi ya kimaendeleo lakini usimamizi wa fedha hizo umekuwa wa kiwango cha juu kwa sababu chama kimekuwa kikifuatilia hatua kwa hatua ili kuhakikisha fedha zote zinatimiza kile kilicholegwa na majengo yanakuwa bora na chama kimejiridhisha vya kutosha.

Pia anatoa wito kwa viongozi kuwa waadilifu kwenye kazi na kuhakikisha kila kitu kinafanywa kwa wakati na kwa thamani ya fedha.

Aidha, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe Joshua Manumbu, anaeleza kuwa wamekamilisha ujenzi wa madarasa katika maeneo mbalimbali na hakuna ulioteteteka kutokana na ushirikiano uliopo kwa viongozi wa eneo hilo na ushirikishwaji wa wananchi. Rasuli Amiri ni Kaimu Ofisa Elimu Wilaya ambaye ni Mratibu wa boost anaeleza kuwa mpango huo utasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani, umbali mrefu wa kutembea akiishukuru serikali akisema mradi wa Boost unaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na kuleta hamasa.

Anaiomba kuona umuhimu wa kuongeza miradi kama hiyo ili kuondokana na tatizo la madarasa na matundu ya vyoo

Kaimu Ofisa Elimu Sekondari, Evarista Msule, anaeleza kuwa kupita miradi hiyo ambayo vyumba vingi vya madarasa vimejengwa na miundombinu kuboreshwa utoro na mimba utotoni vitapungua, tatizo lililokuwa limekithiri katika shule zao.

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Miaka 30 TGNP, ilivyojenga vuguvugu mabadiliko ya usawa wa kijinsia

• Ni kupitia vituo vya taarifa na maarifa

KUWA na taifa lenye usawa wa kijinsia na fursa sawa kwa wote ni harakati za kudumu au endelevu zinazohitaji harakati mbalimbali zinazohusisha asasi za kiraia, serikali na vyombo vya habari mahiri ili kuipigania haki.

Ni lazima kujikita kupigania haki za wote na kukuza ushiriki wa wanawake katika siasa na maendeleo, kwa kuwa kundi hilo ni kama limesahaulika na bado halijachomoza kikamilifu na sauti yake kusikika.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ni miongoni mwa mashiriki yasiyo ya kiserikali yanayoendeleza hatua na harakati za kufikia usawa na sasa unatimiza miaka 30 tangu uanze shughuli za mapambano hayo, huku ukieleza kuwa kwa miongo mitatu, umejenga vuguvugu la mabadiliko katika usawa wa kijinsia na maendeleo, kupitia vituo vyake vya taarifa na maarifa.

Shirika hilo linafanya Tamasha la Jinsia linaloambatana na kutimiza miaka 30 wiki hii katika viwanja vyake vilivyopo Mabibo Dar es Salaam likishirikisha wadau 1,500 kutoka nchi mbalimbali.

Katika semina ya waandishi wa habari Dar es Salaam hivi karibuni yenye lengo la kutambua shughuli za vituo hivyo, Mratibu wa vituo vya taarifa na maarifa, Jacqueline Mtesha, anaeleza umuhimu vituo hivyo katika jamii.

"TGNP inavyo vituo 72 vya taarifa na maarifa katika mikoa 15 na tunaendelea kuongeza vingine zaidi. Vimekuwa ni nguzo muhimu katika ujenzi wa vuguvugu la mabadiliko kwenye jamii hususani katika masuala ya usawa wa kijinsia na maendeleo," anasema Jacqueline.

Anasema kupitia vituo hivyo, Watanzania wamekuwa na mwamko kwa wanawake kujitokeza kwa ujasiri kuwania nafasi mbalimbali za uongozi na pia kutoa taarifa za ukatili unaotokea katika jamii. "Vituo hivi vimesaidia kuijengea uwezo wa jamii wa kupata habari, taarifa na kuendesha au kushiriki mijadala mbalimbali inayohusu utu na usawa wa kijinsia na haki za kijamii," anasema.

Katika ufafanuzi wake anasema kupitia vituo hivyo, watu wamekuwa na uelewa wa kutosha na wanatoa taarifa za vitendo vya ukatili wa kijinsia katika vyombo vya dola, tofauti na miaka nyuma.



Ofisa Mawasiliano wa TGNP, Monica John, alipofungua semina ya waandishi wa habari, kuelekea tamasha la 15 la kijinsia na miaka 30 ya mtandao huo linaloanza leo. **PICHA: SABATO KASIKA**

"Vimeifanya jamii kushiriki mabunge ya wananchi ambayo yanashirikisha viongozi wa maeneo yao na kuibua kero mbalimbali, huku viongozi hao wakizipokea na kuzifanyia kazi changamoto hizo," anasema mratibu.

Anafafanua kuwa katika mabunge hayo, wananchi hujengewa uwezo wa jinsi ya kuwania nafasi za uongozi, ili kuongeza idadi ya wanawake na kwamba jitihada hizo zimezaa matunda katika maeneo mbalimbali na kwamba licha ya kutokuwa na idadi ya wanawake waliochaguliwa katika nafasi za ubunge, udiwani na nyingine baada ya hamasa ya mtandao huo na vituo vyake, anaamini kuwa jamii ina uelewa wa kutosha.

"Mifano ipo mingi ya wanawake ambao wamejengewa uwezo na wakawania uongozi na kushinda. Kwa mfano Kata ya Saranga Kimara Dar es es Salaam, yenye mitaa tisa, mtaa wa King'ongo, mwenyekiti wake ni mwanamama," anasema.

Wakati TNGP ina miaka 30, mratibu huyo anasema vituo vya taarifa na maarifa vina miaka 13 vikianzishwa mwaka 2010 na kuongeza kuwa katika umri huo vimefanya mambo makubwa, vimeleta mafanikio kwa jamii katika maeneo mbalimbali, kwa kuipa jamii hususan wanawake sauti ya kukemea ukatili wa kijinsia, anasema.

Anasema kuwapo kwa vituo hivyo kumesaidia kupeleka maendeleo kwenye maeneo yaliyo nyuma katika nyanja mbalimbali ikiwamo miundombinu ya barabara, shule na hata upatikanaji wa huduma za afya.

**KUHUSU VIKWAZO**

Kila penye mafanikio lazima kuna changamoto zake, licha ya kuwa na mambo mengi ya kujivunia katika miaka hiyo 30, kuna vikwazo mbalimbali, Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Majohe, Tabu Ally anasema na kuongeza kuwa aliwahi kuwekwa ndani na serikali ya mtaa ukiwa ni mkwara wakidhani ana mkakati wa kuwania uongozi.

"Vituo vya taarifa na maarifa, moja ya majukumu yake ni kujengea wananchi uwezo wa kuibua changamoto katika maeneo yao na pia kutoa taarifa za vitendo ambavyo ni kinyume na maadili," anasema Tabu.

Anasema katika juhudi hizo ambazo zinaenda sambamba na kuwafanya wananchi waweze kuhoji mambo ambayo wanaona yanakwenda kinyume, ndipo alikutana na kikwazo hicho.

"Lakini baadaye walielewa lengo la kituo chetu kuwa ni kuwajengea uwezo wananchi ili waibue kero za mtaa wao na vitendo vya ukatili na sasa hakuna tatizo, tunafanya nao kazi kwa ukaribu zaidi ili kupigania maendeleo ya jamii," anasema Tabu.

> Ukweli ni kwamba vituo vya taarifa na maarifavimekuwa msaada mkubwa kwa jamii, ingawa awali vilikutana na changamoto ya kutokukubalika na baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa.

Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa, Kivule, Zahara Mzee anasema awali walipokuwa wanaanza kazi katika jamii, viongozi wa serikali za mitaa hawakuwa na imani nao na kwamba walidhani kuwa wana lengo ya kuwaondoa katika nafasi zao katika uchaguzi.

"Ukweli ni kwamba vituo vya taarifa na maarifa vimekuwa msaada mkubwa kwa jamii, ingawa awali vilikutana na changamoto ya kutokukubalika na baadhi ya viongozi wa serikali za mitaa," anasema.

Zahara anasema kitendo cha kuelimisha jamii ikawa na uwezo wa kuhoji mambo mbalimbali ya maendeleo, kilionekana kana kwamba ni kutaka kuwa kuchukua nafasi za viongozi.

Mtindo wa kutoamini vituo hivyo umewahi kukikumba pia Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kata ya Mabwepande, ambapo mwenyekiti wake Fatuma Nuru, anasema viongozi wa serikali za mitaa waliwalaumu kwa mtindo wao wa kuhoji mambo mbalimbali yanayohusu jamii.

"Baada ya kutambua kuwa lengo letu ni zuri, sasa wanatushirikisha katika vikao vyao vya kujadili maendeleo ya kata yetu ya Mabwepande kwani lengo letu ni kutaka maendeleo ya wananchi kwa kuzingatia usawa wa kijinsia," anasema Fatuma.

SAYANSI
NA GAUDENSIA MNGUMI

# Ujio mkataba wa plastiki hili ni angalizo kwa Afrika

KATIKA dunia ya leo plastiki ni kila kitu. Mosi unaposhuka kitandani saa 11, alfajiri, unawasha taa, swichi na nyaya ni plastiki.

Unaufuata mswaki ni wa plastiki, unauwekea dawa ya meno iko kwenye 'chubu' ya plastiki, unachukua maji ya kunawa, kusukutua na kuuosha yanapitia kwenye bomba la plastiki na mwisho unamaliza kila kitu kwa kuvaa ndala za plastiki na kuingia bafuni.

Unaendelea kutazama huku na kule ili kujua muda, unakimbilia simu yako nayo imeundwa kwa viambato vya plastiki, unapoingia jikoni kufungua kinywa, vyombo vinavyohifadhia sukari majani na hata chupa ya chai ni plastiki.

Ukijiandaa kuondoka, unachukua mafuta, losheni na manukato vipo kwenye mikebe ya plastiki hivyo hata unapojipaka chochote kulainisha ngozi vifungashio ni hivyo hivyo, kwa hiyo, plastiki ni eneo ambalo matumizi yake hayakwepeki.

Lakini, wataalamu wa mazingira wanasema plastiki si salama inaongeza hatari kwenye maisha na hivyo, kutokomeza taka za plastiki ni jukumu kubwa linaloielemea dunia ya leo.

Wetu wanajiuliza kwa nini? Kwa mujibu wa taarifa za Umoja wa Mataifa (UN News), jibu analitoa Inger Andersen, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP), akisema ni kwa sababu taka za plastiki zinaiumiza mifumo ya kiikolojia, tena zinaongeza joto kwenye hali ya hewa na kuna uwezekano mkubwa wa kuharibu afya za binadamu.

Urejelezaji wa taka za plastiki sio mazingaombwe ni lazima ufanyike kwa sababu mifumo haiwezi kuzihimili na kwamba mabadiliko lazima yafanyike katika mzunguko mzima wa maisha ya plastiki.



Rundo la taka za plastiki linalotengenezwa kuonyesha ukubwa wa tatizo hilo dunia. **PICHA: REUTERS**

Anasema ni lazima kuachana nazo, tena watu hawana budi kukataa vitu visivyo vya lazima hasa kwenye vifungashio ili kutumia plastiki kidogo zaidi na pia kuirejeleza.

Wiki iliyopita taasisi ya mawasiliano inayochagiza ulinzi wa mazingira ya Grid Arendal ya Norway, inazungumza na wanahabari katika mkutano mtandao kujadili mkataba wa kimataifa wa kukomesha matumizi ya plastiki duniani.

Lengo la UN la kuwa na mkataba huo wa 'Global Plastic Treaty' ni kukomesha uchafuzi wa taka za plastiki duniani ifikapo mwaka 2040, tena unalenga kupunguza athari za taka hizo kwa kuziingiza kwenye mfumo wa uchumi wa mzunguko ambao utafanikisha plastiki kutumiwa zaidi ya mara moja, kurejelezwa mora pamoja na kusimamia matumizi yake ili kufikia uzalishaji mdogo wa plastiki na kudhibiti zisiingie tena kwenye uchafu wa mazingira na mfumo wa ikolojia.

Thomas Maes mwanasayansi na mtafiti wa masuala ya plastiki anasema uwepo wa plastiki kwenye mazingra ni hatari kuanzia afya za watu na viumbe wengine duniani,

Anasema uzalishaji wa plastiki ni hatari na kwamba kila siku unaongezeka na kukaribia takribani tani bilioni nne ifikapo 2024.

Anaeleza kuwa licha ya kwamba hutumiwa karibu kwenye kila sekta baadhi kwenye kuhifadhi bidhaa na vyakula (chemical additives) plastiki zina kemikali ambazo ni hatari kwa watu na mazingira yao.

Maes anaonya kuwa kama plastiki hazitarejelezwa na kupunguza zaidi matumizi na uzalishaji wake zitasababisha madhara makubwa kwa binadamu.

"Tatizo ni kubwa kwa kuwa kiasi kikubwa hakifanyiwi udhibiti zinaachwa kuzagaa na kuingia kwenye mazingira na kuchafua ikolojia. Plastiki ni bidhaa zinazotengenezwa na binadamu kwa hiyo hakuna sababu ya kuendelea kuziogopa na kwamba dunia nzima karibu udongo wote una plastiki."

Anasema bahari ina taka za plastiki, ziko kwenye kila udongo duniani, ndani ya maji, vina vya bahari na mito na kwamba siyo jambo la kupuuzia tena.

Anasema kuwa ni lazima kukubaliana na ukweli kwamba yapo mataifa ambayo yanazalisha na kuuza plastiki kwa kiasi kikubwa lakini nchi wanazopokea bidhaa hizo hayana uwezo wa kuzirejeleza.

Aidha, yapo mataifa yasiyomudu kudhibiti taka za kawaida zikiwamo za vyakula jikoni, sembuse plastiki na kusema kuwa mkataba huo unataka kuwe na usimamizi wa matumizi, umakini katika ukusanyaji, uchambuzi na kurejeleza na hicho kiwe kipaumbele cha kwanza ikiwa dunia inataka kuwa huru na plastiki.

### HATIMA YA AFRIKA

Mtaalamu wa uhandisi na mhadhiri wa Vyuo Vikuu, Dk. Kamugisha Byabato, akizungumzia mkataba huo na iwapo unaweza kutekelezeka Afrika anasema suala la muhimu ni kupata bidhaa ambayo ni mbadala wa plastiki na si vinginevyo.

Anasema kupata plastiki ambayo ni 'bio-degradable' inayoweza kuliwa kama chakula na vijidudu walioko kwenye mazingira kuanzia ardhini na mwisho kuoza ndiyo ufumbuzi.

Anashauri: "Ni lazima kuanzisha viwanda vyetu vya kuzalisha plastiki au bidhaa nyingine mbadala itakayotumika, kwa sababu hizi tunazotumia leo siyo za kwetu zimetengenezwa ughaibuni."

Anataja kompyuta, simu, runinga, redio, magari, bomba za maji, matairi, vyombo... havijazalishwa Afika vimetoka nje.

Dokta Byabato anayefundisha Chuo Kikuu cha SAUT, Mwanza, anakumbusha kuwa Tanzania na Afrika zinapoingia kwenye mjadala wa kukomesha matumizi ya plastiki ziongozwe na mipango na mikakati ya kuwa na viwanda vyake vya kupata mbadala ambao utapatikana kwa kujenga viwanda vitakavyozalisha kile wanachohitaji si kuwa walaji wa bidhaa za plastiki za viwanda vya nje.

Anaongeza: "Tukisema tunakomesha matumizi ya plastiki ni jambo ambalo haliko kwenye uwezo wetu, sisi ni walaji tu hatuna mbadala. Ikumbukwe plastiki hizo zinazozagaa zinahusisha vifungashio vya bidhaa mbalimbali ambazo hatuzitengenezi, zinatoke nje iwe China, Ulaya na Asia. Lakini pia ni bidhaa ambazo zina viambato (accessories) kama simu, TV, redio..."

Anashauri akisema kuwa nchi zinazoendelea zifikirie kuwa na uwezo wa kuzalisha vitu vyake zenyewe badala ya kutegemea kila bidhaa kutoka nje.

## Shule inavyotumia wahadhiri vyuo vikuu 'kuwakochi', kupenda tahasusi

**INATOKA UK.11**

Anamshukuru Mbunge wa Kisarawe, Selemani Jafo, kwa kushirikiana na uongozi kukabili tatizo la ukosefu wa maji katika shule hiyo.

Anaeleza kuwa awali kulikuwa na kikwazo cha maji lakini kwa sasa wapo wahisani walioletwa na mbunge huyo na kuchimba visima ambavyo vimesaidia upatikanaji wa maji.

"Ninachoomba kwa mbunge wetu Jafo ni kusaidia kupata kisima kingine kikubwa, kama alivyotuwezesha katika hatua hii iliyoleta ahueni atutafutie wadau wengine wa kutuchimbia kisima kikubwa," anazidi kuomba.

### HISTORIA

Akiwa Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe Jokate kwa kushirikiana na Mbunge wa Kisarawe, Selemani Jafo, walifanya harambee iliyowakutanisha wadau mbalimbali wa elimu waliochangia na kufanikisha kuanzishwa kwa sekondari hiyo.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe Mohamed Boniface, anawakumbusha walimu kuzingatia maadili wawapo shuleni ili wanafunzi waige mienendo yao bora.

Anasema walimu ni kielelezo kwa wanafunzi kile watakachokifanya nao watakifuata hivyo kuwa na matendo mazuri na maadili yao itawasaidia kutangaza shule hiyo kuwa bora kimasomo na tabia nzuri pia.

Sambamba na hilo Boniface pia anaelekeza wanafunzi kusoma kwa bidii na kuachana na maneno ya kwenye mitandao ya kijamii ambayo wakati mwingine yanawafanya kukata tamaa ya kuendelea kusoma.

Anasema serikali inaendelea kutatua vikwazo mbalimbali katika sekta ya elimu hivyo wanafunzi wanatakiwa kusimama kwenye nafasi yao ya kuzingatia masomo kitu ambacho ndio kimewapeleka shuleni.

"Kisarawe tunahitaji kuwa na wasomi wengi, hivi vikwazo vilivyopo vinashughulikiwa kila siku na vitaisha hapa ni wanafunzi kusoma kwa bidii " anasisitiza.



## Askofu akemea uvunjifu maadili

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Methodist Tanzania, Joseph Bundala, amewaomba viongozi wa madhehebu ya dini nchini kuunga mkono hatua zilizochukuliwa na serikali za kukemea vitendo vya kuwachezesha watoto nyimbo ambazo hazina maadili ya kitanzania.

Aidha, amewataka wao pia kuhakikisha tabia hiyo inakemewa kwenye makanisa yao ambayo kuna kwaya zinazocheza nyimbo za dini kwa mtindo wa kukata viuno kinyume na maadili ya kiroho.

Hatua hiyo ya Askofu Bundala imekuja baada ya hivi karibuni serikali kupitia Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, kuwasimamisha walimu wakuu wawili wa shule za msingi kutokana na kuwachezesha viuno wanafunzi wadogo nyimbo ambazo hazina maadili.

Askofu Bundala alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na waumini na madhehebu mbalimbali ya dini na viongozi wa chama na serikali waliohudhuria ibada ya kusimikwa kwa Askofu Gabinus Tundwe wa kanisa hilo katika Jimbo la Chamwino, iliyofanyika Mlowa Barabarani wilayani hapa.

Alisema kutokana na hatua iliyoonyeshwa na serikali, viongozi wa madhehebu ya dini wanatakiwa kuunga mkono kwa kuchunguza kwaya zilizopo ndani ya makanisa ambazo zinazohudumu kupitia uimbaji lakini wanakiuka maadili ya kiroho.

"Hatua hii ya serikali kwa kweli inatakiwa kuungwa mkono na viongozi wa makanisa ambayo kuna kwaya ambazo uchezaji wake hauna maadili ya kiroho, kuzipiga marufuku na ikiwezekana kuvunja kwaya hata kama zinaonekana kuwa na mvuto wa waumini ndani ya makanisa haya," alisema.

Pia alisema ndani ya makanisa bado kuna kwaya ambazo hazina maadili ya kiroho katika kucheza kwao, hivyo wanatakiwa kuchunguzwa na wakibainika ziondolewe badala ya kuzifurahia na kuziacha zikiwapotosha watoto.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino, Keneth Yindi, akizungumza kwenye ibada hiyo, alisema serikali itaendelea kushirikiana katika kuchukua hatua za kisheria kwa wale watakaobainika kuchochea vitendo viovu kinyume na utamaduni wa Mtanzania.

Alisema serikali itahakikisha inafanya kazi zake kwa kushirikiana na madhehebu ya dini kwa kuwajengea malezi ya kiroho watoto kuanzia ngazi ya chini ili taifa liweza kuwa na Watanzania wenye hofu ya Mungu.

"Sisi viongozi serikali tutahakikisha tunaungana na kanisa hili katika kukemea na kuelimisha umuhimu wa malezi ya kuwaandaa watoto ili waweze kuwa viongozi ndani ya nchi hii ambao watakaokuwa na hofu ya Mungu na kuipenda nchi na watu wake na rasilimali zake," alisema.

# Wafugaji wataja mwarobaini wa migogoro baina yao na wakulima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

CHAMA cha Wafugaji Tanzania (CCWT) kimefichua mwarobani pekee ambao utasaidia kumaliza migogoro ya wafugaji na wakulima ambayo imekuwa ikisababisha mauaji katika maeneo mbalimbali nchini.

Makamu Mwenyekiti wa CCWT, Kusundwa Wamalwa, alisema hayo jana jijini hapa, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwenye kikao cha kumtambulisha mlezi wa chama hicho, Joseph Makongoro.

Wamalwa alisema mwarobaini pekee wa kumaliza migogoro baina ya wafugaji na wakulima ni serikali kupima na kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za ufugaji.

"Kama serikali itapima maeneo na kuyatenga kwa ajili ya wafugaji, itasaidia kumaliza hii migogoro ya muda mrefu baini ya jamii hizi mbili ambazo zimekuwa zikifanyiana uhasama ambao wakati mwingine unasababisha watu kupoteza maisha," alisema.

Pia alisema njia nyingine ya kukomesha migogoro hiyo ni serikali kuifanyia kazi ripoti iliyondaliwa na jamii za wafugaji ikiwa chini ya Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka na kupelekwa bungeni ikiwa na mapendekezo mbalimbali.

Alisema moja ya pendekezo katika ripoti hiyo ilikuwa mapori yote ambayo hivi sasa yamepoteza sifa yatolewe kwa wafugaji ili wayatumie kwa ajili ya malisho ya mifugo yao.

"Hali hii pia itasaidia kuondoa migogoro baini ya wafugaji na askari wa mapori ya akiba pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) ambao wamekuwa wakiwanyanyasa wafugaji pale mifugo yao inapoikingia kwenye maeneo hayo na kupelekea wafugaji kuuawa kwa kupigwa risasi," alisema Wamalwa.

Katibu Mkuu wa CCWT, Daniel Mathayo, alisema hivi sasa wanaendelea na usajili wa wafugaji nchi nzima ili kupata idadi yao pamoja na mahitaji yao ili kuyafikisha serikalini yafanyiwe kazi.

"Nitoe wito kwa wafugaji wote kujitokeza katika usajili kwa njia ya kielektroniki ambayo itawawezesha wafugaji kutambulika idadi yao ili mahitaji yao yafanyiwe kazi kupitia chama chetu na serikali pia kupitia Wizara ya Mifugo," alisema.

Naye mlezi wa CCWT, Joseph Makongoro, alisema kipaumbele chake ni kuhakikisha migogoro baina ya wafugaji na wakulima inakwisha nchini.

"Wafugaji na wakulima ni watoto wa mama mmoja na baba mmoja. Sioni sababu za kuendelea kugombana, hivyo nikiwa mlezi na kwa kushirikiana na CCWT na serikali yetu chini ya Rais Samia Suluhu Hassan, nitahakikisha kuwa tunamaliza migogoro yote ili kuongeza tija katika sekta ya mifugo nchini," alisema.

Awali, Mwenyekiti wa CCWT, Mrida Mshota, akimtambulisha kwa waandishi wa habari mlezi huyo, alisema lengo la chama hicho ni kusajili wafugaji zaidi ya milioni nne.

"Usajili huu utatusaidia sisi kama chama, lakini serikali kuwa na idadi sahihi ya wafugaji ili kuweza kufanyia kazi changamoto zote zinazowakabili," alisema.



Baadhi ya wageni kutoka maeneo mbalimbali nchini wakiwa ndani ya ukumbi wa Bunge jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Madiwani walalamika mradi maji kutokamilika

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni mkoani Singida, wameulalamikia Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) wilayani hapa kutokana na mradi wa maji wa Kintinku-Lusilile unaojengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 12 kuchukua muda mrefu kukamilika. Madiwani hao walitoa malalamiko hayo mwishoni mwa wiki katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani cha robo ya kwanza cha mwaka wa fedha 2023/24 wakati wakijadili taarifa ya RUWASA.

Katika kikao hicho ambacho pia kilihudhuliwa na Mbunge wa Manyoni Mashariki, Dk. Pius Chaya, madiwani hao walishangazwa mradi huo utakaohudumia vijiji 12 kutokamilika kama mkataba ulivyosainiwa.

Walisema kwa mujibu wa mkataba ujenzi wa mradi huo ilikuwa ukamilika Novemba, mwaka huu, lakini katika hali ya kushangaza umesogezwa hadi Januari, mwakani huku wananchi wakiendelea kupata adha ya ukosefu wa majisafi na salama.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Jumanne Mlagaza, aliwataka madiwani kusimamia vyema miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kuhakikisha miradi hiyo inakidhi thamani ya fedha iliyotolewa na serikali.

"Serikali inatoa fedha nyingi kwa ajili ya ujenzi wa miradi hii fuatilieni kwa ukaribu kwani kumekuwa na udanganyifu kwenye baadhi ya maeneo ambapo mara kadhaa miradi hukamamilika na kukabidhiwa ikiwa haijakidhi vigezo pamoja na thamani halisi," alisema.

Aidha, baraza hilo lilitangaza kumfuta kazi Muuguzi Msaidizi, Atieno Otieno, kwa sababu za utoro kazini.

Mlagaza alisema baraza hilo limefikia hatua hiyo baada ya kubaini kuwa mfanyakazi huyo aliyekuwa akifanya kazi katika Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya hiyo ameenda kinyume cha sheria.

"Kwa mujibu wa sheria mtu anapokosekana siku tano katika kituo chake cha kazi bila ya kuwepo kwa taarifa yoyote anakuwa amekiuka mashariti, hivyo kuanzia leo kikao hiki cha madiwani kimeridhia kumfukuza kazi na kuanzia sasa Atieno sio mfanyakazi wa halmashauri hii," alisema.



# Polisi yaonyesha utayari kukabili uhalifu Mbeya

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, limeanza matembezi maalumu ya kuonyesha mbinu mbalimbali za kukabiliana na uhalifu ikiwamo maonyesho ya silaha za kivita pamoja na kuzungumza na wananchi.

Jeshi hilo lilifanya maonyesho hayo mwishoni mwa wiki ambapo zaidi ya maofisa na askari polisi 300 kutoka katika wilaya zote za mkoa, walishiriki matembezi hayo ambayo yalifanyika katika mitaa mbalimbali ya Jiji la Mbeya na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Akizungumza baada ya maonyesho hayo, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi (ACP) Benjamin Kuzaga, alisema lengo lingine la maonyesho hayo lilikuwa kujiweka sawa katika kukabiliana na matukio ya uhalifu. Pia alisema aliamua kuwakumbusha askari na maofisa mbinu za medali za kivita ili ziwasaidie kwenye kukabiliana na matukio mbalimbali ya uhalifu ambayo yamekuwa yakiibuka mitaani.

"Lakini tunalenga kuongea na wananchi kuhusu masuala ya ulinzi na usalama katika maeneo yao ya makazi na kwenye maeneo ya shughuli zao za kujiingizia kipato ikiwamo maeneo ya biashara," alisema.

Kamanda Kuzaga alisema walikuwa wanaonyesha vifaa mbalimbali vya kivita yakiwamo magari, bunduki na kufanya doria za kutembea kwa miguu katika mitaa mbalimbali na kwamba wataendelea kufanya maonyesho hayo kwenye maeneo mbalimbali na kuwaelimisha wananchi namna ya kushiriki kukabiliana na uhalifu.

Aliwataka askari kuendelea kufanya kazi kwa weledi ikiwa ni pamoja na kuzingatia miiko ya kazi yao huku akiwataka askari kata kufanya kazi kwa kushirikiana na viongozi wa serikali wa maeneo yao.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa maonyesho hayo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alilitaka Jeshi la Polisi mkoani hapa kuchukua hatua za kisheria dhidi ya watu wote wanaoingilia utendaji kazi wa jeshi hilo.

Moja ya makundi ambayo Homera alitaka yashughulikiwe ni pamoja na wanaharakati ambao wamekuwa wakikwamisha shughuli za jeshi hilo kwa njia mbalimbali.

Homera alisema baadhi ya wanaharakati na wanasiasa hao wamekuwa wakitumia lugha za matusi, kukashfu viongozi wa nchi na Jeshi la Polisi na hivyo akawataka kuacha mara moja tabia hiyo kwa maelezo kuwa watachukuliwa hatua kali.

"Shughulikeni na watu hao. Haiwezekani mtu anatukana matusi hadharani halafu anaachwa hivi hivi. Msiwafumbie macho hawa watu wanaoharibu taswira ya mkoa wetu," alisema.

Homera alipongeza kazi inayofanywa na vikosi vyote vya Jeshi la Polisi kuhakikisha ulinzi na usalama wa raia na mali zao unakuwapo na wananchi kufanya kazi zao za maendeleo bila bugudha wala wasiwasi wowote.



Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samwel Gwamaka (kushoto), akiwa na baadhi ya maofisa wa Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Rukwa pamoja wajumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya walipofanya ziara ya kuangalia uharibifu wa mazingira unaofanywa na wachimbaji wa madini kwenye Mto Zira wilayani humo, mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## TRA yavuka lengo ukusanyaji mapato

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

MENEJA wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Njombe, Specioza Owure, amesema mkoa umekusanya Sh. bilioni 4.6 kwenye Robo ya Kwanza ya Mwaka wa Fedha 2023/24 sawa na asilimia 101 ya lengo la makusanyo.

Amesema mkoa huo umepangiwa kukusanya Sh. bilioni 16.3 kwa mwaka na kila robo wanatakiwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 4.1 ili kufikia lengo.

Owure aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya pamoja kati ya TRA na wafanyabiashara wa Halmashauri ya Mji Makambako. Alisema moja ya mafanikio hayo ni kuvuka robo ya kwanza ya makusanyo.

"Na pia tumevuka malengo kutoka mwaka wa fedha Julai mpaka Oktoba. Kwa sasa tuna asilimia 101 na hii yote ni kwa sababu ya ushirikiano tulio nao na walipakodi," alisema Owure.

Akizungumzia uwapo wa mashine bandia, meneja huyo alisema hadi sasa wameshafungia mashine za baadhi ya wafanyabiashara ili zisiendelee kufanya kazi.

"Lakini tuna mashine mbili ambazo zilikuwa zinafanya shughuli hizo ambazo tumezinasa. Kwa hiyo hicho kitu kipo na tunaendelea kuelimishana. Tunaendelea kuomba ushirikiano ili kuwafichua hao watu wote na hicho kitu kisiwapo kabisa katika mkoa wa Njombe," alisema Owure.

Mkuu wa Wilaya ya Njombe, Kissa Kasongwa, alisema kumekuwa na changamoto kwamba kuna watu wanakwepa kodi na hawalipi kodi.

"Nimefurahi kwamba katika Wilaya ya Njombe, kwenye mkoa wote wa Njombe, sisi ndio ambao tunakusanya zaidi ya asilimia 90 ya mkoa wa Njombe wote. Kwenye wilaya ya Njombe tunatarajia kukusanya bilioni 14 halafu wilaya nyingine zote tatu wenyewe wanachangia Sh. bilioni mbili mpaka sasa kwenye robo ya kwanza tumeshakusanya Sh. bilioni nne," alisema Kasongwa.

Kasongwa alisema serikali inapata changamoto kutoka kwa wafanyabiashara kuhusu suala sugu za utoaji wa risiti pindi wanapouza bidhaa.

# Vijiji 24 kunufaika matumizi bora ya ardhi

**Na Elizabeth John,**
WANGING'OMBE

VIJIJI 24 vya wilaya nne za mikoa ya Mbeya, Njombe na Iringa, vinatarajiwa kunufaika na mpango bora wa matumizi ya ardhi ambao unakwenda sambamba na kupima maeneo ya uhifadhi ili kulinda vyanzo vya maji na kupunguza migogoro ya ardhi.

Vijiji vitakavyonufaika na zitakazonufaika na mradi huo kutoka Wilaya za Mbeya (Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya) na Mbarali kwa mkoani Wanging'ombe mkoani Njombe na Iringa (Halmashauri ya Wilaya ya Iringa).

Meneja wa Tume ya Taifa ya Mpango ya Matumizi Bora ya Ardhi Kanda Nyanda za Juu Kusini, Pili Msati, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari wilayani hapa.

Msati alisema serikali imeamua kutoa huduma hiyo kwa wananchi ili kuhakikisha vijiji vyote vinapangwa vyema na kuainisha maeneo muhimu katika vijiji yakiwamo ya makazi, malisho, kilimo na uhifadhi katika vijiji vyao ili kutunza uoto ambao umeelezwa umeanza kupotea.

"Tume inafanya kazi hii kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kwamba kupitia mradi wa urejeshaji wa uoto wa asili pamoja na utunzaji wa mazingira ikiwamo misitu na vyanzo vya maji," alisema Msati.

Aidha, Msati alisema hivi sasa hatua inayofuata ni kuwamilikisha wananchi katika maeneo ambayo yanaonekana kwamba ni muhimu kwa ajili ya uhifadhi wa mazingira.

"Na kwa Wilaya ya Wanging'ombe pia kuna Kijiji cha Mapogolo ambacho chenyewe tunaanza na hatua ya kwanza kabisa ya upangaji matumizi," alisema Msati.

Mtaalamu kutoka Tume ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, Heroni Chaka, alisema moja ya vitu ambavyo wamekishuhudia katika Kijiji cha Mapogolo ni wananchi kuwa na shauku kwa sababu vijiji jirani vilikuwa vimeshafanyiwa mpango wa matumizi ya ardhi.

"Katika kuandaa mpango huu wa matumizi ya ardhi katika kijiji cha Mapogolo changamoto kubwa ilikuwa mwingiliano wa matumizi katika vijiji vya Mapogolo na Ukomola lakini tatizo hilo tumefanikiwa kulitatua," alisema Chaka.

Mpimaji wa ardhi kutoka wilaya ya Wanging'ombe, Albert Mwakipesile, alisema mpango huo wa matumizi bora ya ardhi, una manufaa mengi kwa wananchi wa wilaya hiyo.

"Mpango huu unasaidia kutatua matatizo ya mipaka ya kijiji na kijiji mtu na mtu na baada ya mipango yote kukamilika. Mtu akapangiwa eneo lake akapata hati ile ya kimila na inamsaidia kupata mikopo benki," alisema Mwakipesile.

Baadhi ya wananchi wa kijiji cha Mapogolo, wameipongeza serikali kwa kuanza kuweka mpango bora wa matumizi ya ardhi katika kijiji hicho.

"Wananchi kwanza tumeupokea kwanza huu mpango,pili tutafaidika kwenye mambo mengi ikiwemo kutunza kwa urahisi vyanzo vya maji ili kupata maji kwa wingi," alisema Sara Kifikiro, mmoja wa wananchi wa kijiji hicho.

Naye Fadiri Mvinile alisema wametenga maeneo ambayo yatasaidia kuondokana na migogoro kati ya wafugaji na wakulima.





# Tanzania yajizatiti kuimarisha sekta afya

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema serikali ya Muungano na ya Zanzibar, zitaendelea kuhakikisha mipango ya sekta mbalimbali ikiwamo ya afya, inafanikiwa kwa weledi mkubwa kwa kusimamia huduma kuwafikia wananchi katika maeneo tofauti nchini.

Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, alisema hayo juzi kwenye Mkutano Mkuu wa Nne wa Chama cha Wataalamu wa Viungo na Vifaa Tiba Saidizi (APOT) unakwenda sambamba na kilele cha Siku ya Wataalamu wa Viungo na Vifaa Tiba Saidizi Duniani uliofanyika katika Ukumbi wa Sheikh Idris Abdul- Wakil, Kikwajuni Zanzibar.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya ina dhamana kubwa ya kusimamia masuala yanayohusu watu wenye ulemavu wa viungo, uhitaji wao na kuhakikisha huduma bora zinawafikia kwa ukaribu zaidi kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali ya Muungano imetunga Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma za Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 na Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya 2010 kuhakikisha haki za watu wenye ulemavu zinazingatiwa sambamba na kuimarisha miundombinu rafiki kwa ajili yao.

Alisema sheria hiyo imeelekeza jinsi ambavyo watu wenye ulemavu watapewa kipaumbele kwenye masuala ya ajira, fursa na nafasi katika kupata huduma na kujumuika na jamii sambamba na kupinga unyanyasaji wa aina yoyote ile kwa watu wenye ulemavu.

Pia alisema katika kukabiliana na upungufu wa wataalamu wa kutoa huduma za viungo tiba na vifaa saidizi nchini serikali kupitia Wizara ya Afya imeajiri wataalamu katika hospitali za rufani za mikoa, kanda, hospitali za taifa na za Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ).

Alisema pia serikali imeandaa na kuzindua mpango mkakati wa huduma za utengamano na tiba shufaa ambao utaimarisha huduma za utengano na kuwataka watendaji wa afya na wananchi kuusoma na kutoa maoni na mapendekezo yatakayofanikisha utekelezaji mzuri wa mpango mkakati uliopitishwa.

Naibu Waziri wa Afya, Hassan Khamis Hafidh, aliutaka umoja wa wataalamu wa viungo na vifaa tiba saidizi kutoa fursa sawa kwa wanachama wote hasa katika masuala ya kujiendeleza kielimu na utoaji wa huduma bora.

Hassan alisema watu wenye ulemavu wamepewa kipaumbele na nafasi maalumu katika masuala ya ajira na kuwataka kuomba ajira hizo zinapotangazwa .

Akizungumza kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya ya serikali ya Mungano, Omar Kibuyu, aliwataka wanataaluma kutanua wigo katika kufanya kazi za kuwasaidia wenye uhitaji wa vifaa tiba saidizi sambamba na kujiendeleza katika taaluma hiyo ili kupunguza uhaba wa wataalamu wa kutengeneza na kutoa matibabu ya vifaa tiba saidizi nchini.

Raisi wa Chama cha Wataalamu wa Viungo na Vifaa Tiba Tanzania, Exaud Kasegezya, alisema chama hicho kimeanzisha mpango wa upatikanaji wa vifaa tiba katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na Chakechake, Pemba pamoja na kuwapatia ufadhili wa masomo kwa wataalamu wanaojiendeleza na shahada ya pili katika kada hiyo.

Alisema licha ya mafanikio hayo, chama hicho kinakabiliwa na changomoto ikiwemo kutokuwapo kwa kurugenzi ya huduma ya utengamano katika ngazi ya wizara, hospitali za rufani za mkoa na wilaya jambo ambalo linazorotesha upatikanaji wa huduma bora ya tiba ya viugo na vifaa saidizi.




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga (katikati), akishuhudia Ofisa Mkuu wa Fedha NMB, Juma Kimori (kushoto), akiwa na Kamishna wa Idara ya Mashirikiano ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi Zanzibar (ZPPP), Dk. Bill Kiwia, wakitia saini hati ya makubaliano ya kuimarisha miundombinu ya uwekezaji Zanzibar na kujenga mazingira mazuri kwa wawekezaji. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bodi ya ZEMA yatwishwa zigo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WATENDAJI wa Bodi ya Mamlaka ya Mazingira (ZEMA) wametakiwa kutunza mazingira na kuhakikisha viumbehai pamoja na misitu inalindwa ili kuepuka uharibifu.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Harusi Said Suleiman, alisema jana wakati akizungumza na watendaji wa bodi mpya ya mazingira na kuipa majukumu yake.

Alisema Zanzibar inakabiliwa na uharibifu wa mazingira ambao unatokana na mabadiliko ya tabianchi na athari nyingi zimejitokeza.

Harusi alizitaja athari zinazojitokeza kutokana na mabadiliko ya tabianchi kuwa ni pamoja na kasi ya maji ya bahari kuvamia maeneo ya fukwe na kusababisha madhara kwa wananchi.

Alisema baadhi ya maeneo ya fukwe za ukanda wa bahari ikiwamo katika visiwa vidogo vidogo wananchi wake wameanza kuyakimbia kutokana na mmomonyoko wa bahari.

Pia alisema uvuvi haramu ni tishio kwa maisha ya viumbe wa baharini ambapo juhudi zinahitajika katika kulipatia ufumbuzi tatizo hilo.

"Hizo ndizo changamoto zinazoikabili Zanzibar katika masuala ya uharibifu wa mazingira katika maeneo ya ukanda wa fukwe pamoja na bahari kwa ujumla," alisema.

Mwenyekiti wa Bodi ya ZEMA, Asha Ali Khatib, aliwataka wananchi kulinda mazingira ya baharini na nchi kavu kwa ajili ya faida ya vizazi vijavyo.

Aliyataja baadhi ya matukio yanayotishia uharibifu wa mazingira kuwa ni pamoja na uchimbaji wa mchanga unaofanywa na wananchi katika maeneo mbalimbali ya visiwa vya Unguja na Pemba.

Zanzibar, alisema inakabiliwa na tishio la uhaba wa mchanga kutokana na kuwapo kwa matumizi holela na wananchi kujichimbia mchanga bila ya kufuata maelekezo sahihi.

"Kumejitokeza matukio makubwa ya uharibifu wa mazingira katika maeneo mbali mbali ikiwemo ukataji wa miti pamoja na mazingira ya baharini yanayowahusu moja kwa moja samaki na matumbawe," alisema.

# Uchumi wa buluu waongeza nafasi za ajira

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Uvuvi wa Bahari Kuu, imesema mpango wa uchumi wa buluu umefungua mlango wa ajira tangu kuanza utekelezaji wake baada ya kuanzishwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Dk. Emannuel Sweke, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu utekelezaji wa mpango wa uchumi wa buluu katika kipindi cha miaka mitatu tangu Rais Mwinyi kushika wadhifa huo.

Alisema kasi ya usajili wa meli za uvuvi wa bahari kuu imekuwa ikiongezeka baada ya mamlaka hiyo kutoa leseni 100 za uvuvi wa bahari kuu zikiwamo za kampuni za kimataifa.

"Kuna ajira za moja kwa moja ambazo zimesaidia kufikia lengo la serikali katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kutoa ajira 300,000 kwa wananchi wa Zanzibar katika kipindi cha miaka mitano cha serikali ya awamu ya nane," alisema.

Dk. Sweke alisema mpaka sasa mabaharia 14 kutoka Zanzibar na Tanzania Bara wameajiriwa katika meli za uvuvi wa bahari kuu na tayari wawekezaji kutoka nje na ndani ya nchi wameanza kujitokeza kuwekeza katika sekta hiyo.

Pia alisema mchakato wa kuanzishwa kiwanda cha kuchakata minofu ya samaki umeanza kufanyika na zaidi ya ajira 100 zinatarajiwa kutolewa mbali na wachuuzi ambao watanufaika na samaki watakaotayarishwa na kiwanda hicho.

"Katika mwaka wa fedha 2019/20 hatukutoa leseni hata moja ya uvuvi wa bahari kuu kutokana na mazingira yaliokuwa yamejitokeza yakiwamo maradhi ya corona lakini kuanzia mwaka 2020 hadi 2023 tumetoa leseni 100 kutoka leseni 30 zikiwamo za kampuni za uvuvi za kimataifa," alisema Dk. Sweke.

Alisema tangu kuanzishwa kwa mamlaka hiyo mwaka 2010, sekta ya uvuvi imeanza kuchangia kiwango kikubwa pato la taifa hasa baada ya kuanzishwa mpango wa uchumi wa buluu wa kuongeza uzalishaji kupitia maliasili za baharini.

Kwa mujibu wa sheria ya mamlaka hiyo, alisema Serikali ya Muungano imekuwa ikinufaika na asilimia 30 ya mapato, asilimia 20 serikali ya Zanzibar na asilimia 50 hunufaika Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania.

Dk. Sweke alisema mbali na kutoa leseni za uvuvi wa bahari kuu, pia mamlaka ina jukumu la kuhakikisha meli za uvuvi zinazingatia uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa usalama wa rasilimali zake.

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.118 OF 2023**
**IN the Matter of the late:**
**LUKA ROKI CHAMAYOMBE**

**By 1.EDNA LUKA CHAMAYOMBE**
**2.............................................**

ALL persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate(or letter of administration) is made to the above-named pepetitioner.
Objection to the grant should be filed on or before the 27 day of November 2023.
Dated at Morogoro this 02 day of November 2023.

..................................
**RESIDENT MAGISTRATE**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ERICK TRIPHONE MBITA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P.3093/092** kilichotolewa na **KANANURA SEKONDARI CENTRE** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/ILA/11076/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OPTATUS LAURENT MTALO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 909 ACD – PICK-UP HILUX.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/PWA/BAG/3084/2023.**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya...........TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA...........Mkoa...TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na................196/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: MICHAEL JOHN FARU**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: JOHN FARU MICHAEL**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 8 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
ImetolewaleoTarehe ....2... mwezi ...11...mwaka 2023

Imetolewa leo Tarehe ....2.... Mwezi ..11.. Mwaka ..2023
HAKIMU
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya...........TANGA**

**Kituo cha MJINI TANGA...........Mkoa...TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi Na................193/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: SINDI ISMAIL HASSANI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: MWALIMU SINDI ISMAIL**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo tarehe 15 Mwezi 11 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
*Marehemu hakuacha wosia
ImetolewaleoTarehe ....1... mwezi ...11...mwaka 2023

Imetolewa leo Tarehe ....1.... Mwezi ..11.. Mwaka ..2023
HAKIMU
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI TANGA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MUNA SAID AWADH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 612 DUW** aina ya **NISSAN DUALIS.** Chassis namba **J10094800**. Engine namba **MR20390708A**. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu.
**Taarifa ya Polisi: PHQ/DAR/KIN/30803/2023.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**GOLDI KERENGE** anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo cha DEGREE OF BACHELOR OF SCIENCE IN APPLIED GEOLOGY kilichotolewa na THE UNIVERSITY OF DODOMA mwaka 2018. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA: PHQ/MOR/GAI/5559/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**EVA MWAKUJONGA** anatangaza kupotea kwa cheti cha ualimu Grade A chenye usajili namba **E0567-0013** kilichotolewa na **MONTESSORI KAWEKAMO TEACHERS' COLLEGE** mwaka 2016. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MWA/NY/RB/217878/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IBRAHIM - MAANYA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye jina la **MASUNOOR ENTERPRISES (T) LTD** namba za usajili **T 601 AKW** aina ya Toyota Chaser. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/DOD/DOD/7779/2023**


## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**LEONARD HERUMAN MREMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 562 BPU** aina ya **TOYOTA FIELDER** yenye Chassis **No. ZZE1220042426.** Engine **No. 1ZZ9261657.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/6315/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDALLAH RISASI RAJABU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 384 DMN** aina ya **SUBARU FORESTER.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/6100/2023.**

## KUPOTEA KWA VYETI



**KABULA GODFREY KIBINZA** anatangaza kupotea kwa **LEAVING CERTIFICATE** ya kidato cha nne iliyotolewa na **UBUNGO MODERN SEKONDARI** mwaka 2008. Cheti cha Chuo **BUSINESS ADMINISTRATION** chenye namba 01579 kilichotolewa na **KILIMANJARO INSTITUTE OF TECHNOLOGY MANAGEMENT** mwaka 2018. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **PHQ/DAR/KIN/36065/2023.**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA YA NACHINGWEA,MKOA WA LINDI.**

**KUITWA SHAURINI.**

NDUGU MAIKO BANARBA MAPUA UNAAMRIWA KUHUDHURIA MBELE YA BARAZA LILILOPO JENGO LA MJI MDOGO WILAYA YA NACHINGWEA, SHAURI LIMEPANGWA KUTAJWA TAREHE 16/2023 SAA 2;00 ASUBUHI.

SIKU HIYO USIPOUDHURIA SHAURI LITASIKILIZWA UPANDE MMOJA NA KUAMURIWA DHIDI YENU.

AMRI HII IMETOLEWA NA REBECA MJANJA.
**MWENYEKITI BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA.**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**OFISI ZA MATANGAZO Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 0677020701**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**
**Website: www.ippmedia.com**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Israel yaigawa Gaza kusini na kaskazini

**Na Maulid Mmbaga**

**Hata hivyo, mauaji zaidi ya kutisha dhidi ya raia wa Gaza, inaghadhabisha, sawa na kuzuia chakula, maji, dawa, umeme na nishati kuwafikia Wapalestina milioni 2.2, siku 30 zimepita, hii lazima ikome sasa.**

ISRAEL imesema mashambulizi yake ya anga katika ukanda wa Gaza yamefanikiwa kugawa ardhi hiyo ya Palestina kwa sehemu mbili Kaskazini na Kusini, huku ikiahidi mashambulizi zaidi ambayo yataendelea siku zijazo.

Takriban maeneo 450 yamepigwa katika Ukanda wa Gaza, lakini inaelezwa kuwa lengo kuu la mashambulizi hayo lilikuwa kaskazini magharibi na kusini mwa Gaza ambako Israel inapanua operesheni yake ya ardhini.

Mkurugenzi wa Hospitali ya Al Shifa ya Gaza City, ambaye alifanyiwa mahojiano na BBC anasema takribani watu 200 wameuawa katika migomo iliyofanyika usiku kucha, huku karibu 100 wakijeruhiwa huko katikati mwa Ukanda wa Gaza, akieleza kuwa huwenda idadi hiyo itaongezeka.

Msemaji wa Jeshi la Israel, Daniel Hagari, anasema kwamba wanajeshi wa taifa hilo, wamezunguka mji wa Gaza, na kwa sasa wanaendeleza mipango yao ya kijeshi.

Aidha, inaelezwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, ameendelea na ziara ya kanda ya mashariki ya kati, kwa ajili ya kukabiliana na tishio la mgogoro huo kusambaa katika kanda nzima.

Inabainishwa kuwa Waziri Blinken, amekutana na Rais wa Palestina, Mahmoud Abbas katika eneo linalokaliwa na Israel la ukingo wa magharibi, pamoja na viongozi wengine akiwamo Waziri Mkuu wa Iraq, Mohammed Al-Sudani, kwa lengo la kujadili mgogoro huo na kuona umuhimu wa kuzuia vita kusambaa.

Baada ya kukutana na viongozi hao Waziri Blinken ameshutumu mauaji ya halaiki yanayotekelezwa na Israel katika Ukanda wa Gaza. Akisema mapigano yanapaswa kusitishwa mara moja na misaada ya kibinadamu inapaswa kuingia katika ukanda huo.

Wakati hayo yakiendelea, Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, amefutilia mbali wito huo wa usitishwaji wowote wa mapigano hadi mateka wa Hamas watakapoachiliwa.

Pia Jeshi la Israel limeonya kwamba mashambulizi makubwa yataendelea katika siku zijazo huko Gaza, eneo ambalo sasa limegawanywa mara mbili kati ya Gaza Kusini na Gaza Kaskazini.

**FAMILIA YATEKETEA**

Hata hivyo, inaelezwa kuwa watu wanne wa familia ya mwandishi wa habari wa Lebanon, wakiwamo watoto watatu na mwanamke mmoja, waliuawa na shambulio la Israel kwenye gari lao kusini mwa Lebanon.

Katika kulipiza kisasi, Hezbollah inadaiwa kuwa ilirusha makombora huko Kiryat Shmona, kaskazini mwa Israel na inatarajia kuwasilisha malalamiko yake kwa Umoja wa Mataifa (UN).

**MWANAJESHI ACHOMWA KISU**

Katika hatua nyingine inabainishwa kuwa Mwanajeshi wa Israel amejeruhiwa vibaya baada ya kuchomwa kisu katika eneo la Jerusalem Mashariki eneo linalokaliwa kwa mabavu, karibu na lango la Mji Mkongwe.

Polisi wa Israel wanasema mshambuliaji huyo anayeshukiwa kuwa na umri wa miaka 16 kutoka eneo la Issawiya mjini humo, amepigwa risasi na kuuawa na vikosi vya usalama baada ya kuwadunga kisu watu wawili akiwamo mwanajeshi kwenye mtaa wa Sultan Suleiman, na kwa kwamba mshukiwa wa pili amekamatwa na uchunguzi unaendelea.

Huduma ya dharura ya Israel ya Magen David Adom (MDA), imethibitisha kuwa mwanamke mwenye umri wa miaka 20 amepelekwa hospitali kwa matibabu akiwa na majeraha mabaya.

**MSAADA WA JORDAN**

Wakati misaada zaidi ikihitajika huko Gaza, Jordan imeunga mkono jitihada za kuwasaidia wakazi wa ukanda huo baada ya kudondosha misaada kwa parachute iliyoelekezwa katika hospitali zinazohudumia majeruhi.

Pia Israel inasema kudondoshwa kwa misaada ya anga ya Jordan huko Gaza ilitekelezwa kwa ushirikiano na Jeshi la Ulinzi la Israel.

Mfalme wa Jordan Abdullah II, anasema jeshi la anga la nchi yake limetupa vifaa vya matibabu na chakula katika hospitali ya Jordan huko Gaza, akisema ni jukumu la jeshi lake kusaidia majeruhi ambao walikuwa wakiteseka katika ukanda huo.

Tangu Oktoba 7, zaidi ya Waisrael 1,400 waliuawa, wakiwamo wanajeshi 341 na Jeshi la Israel linaripoti watu 240 wanaoshikiliwa mateka na Hamas. Huku Wizara ya Afya ya Hamas ikitangaza idadi ya vifo vya Wapalestina 9,770 wakiwamo watoto 4,800.

**UN**

Wakuu wa mashirika kadhaa ya Umoja wa Mataifa wametoa wito wa pamoja wa kutaka usitishaji vita mara moja kati ya Israel na kundi la wanamgambo la Hamas katika Ukanda wa Gaza.

Kupitia taarifa ya pamoja, wakuu hao wamerudia wito wao kwa pande husika kwenye vita hivyo kuheshimu wajibu wao chini ya sheria ya kimataifa kuhusu haki za kibinadamu na huduma za kiutu.

Inaelezwa kuwa miongoni mwa wakuu waliotoa taarifa hiyo ni kutoka shirika linaloratibu misaada ya kiutu (OCHA), Shirika la Mipango ya Kimaendeleo la UN, Shirika la kuwashughulikia wahamiaji (UNHCR) na mashirika ya kimataifa yanayotoa misaada ya 'Save the Children na Care International'.

Taarifa yao inalaani kile walichokiita mauaji ya kutisha ya Waisrael, utekaji nyara uliofanywa na wanamgambo wa Hamas na makombora yanayofyatuliwa kutoka Gaza.

"Hata hivyo, mauaji zaidi ya kutisha dhidi ya raia wa Gaza, inaghadhabisha, sawa na kuzuia chakula, maji, dawa, umeme na nishati kuwafikia Wapalestina milioni 2.2, siku 30 zimepita, hii lazima ikome sasa," taarifa hiyo imesema. **Chanzo mashirika ya kimataifa**

## Museveni apuuzia Uganda kuondolewa AGOA

**KAMPALA,**

RAIS wa Uganda, Yoweri Museveni, ameonyesha kupuuzia mbali wasiwasi wake kuhusu kuondolewa kwa nchi yake katika mpango maalum wa kibiashara wa Marekani na Afrika (AGOA).

Siku chache zilizopita, Rais wa Marekani Joe Biden, alisema Uganda na nchi nyingine tatu za Kiafrika zitaondolewa kwenye mkataba wa AGOA, akitoa mfano wa Uganda inayodaiwa kuwa mkiukaji wa haki za binadamu zinazotambuliwa kimataifa.

Licha ya angalizo hilo, Rais Museveni aliikosoa Marekani, akisema wanajiona bora kupita kiasi na kimakosa wanafikiri kwamba nchi za Afrika haziwezi kusonga mbele bila uungwaji mkono wao.

"Kama Uganda inavyohusika, tuna uwezo wa kufikia malengo yetu ya ukuaji na mabadiliko, hata kama baadhi ya wahusika hawatuungi mkono," alisema Rais Museveni.

Aidha, ilielezwa kuwa Marekani imetaka kuchukua hatua dhidi ya Uganda, ambayo mwezi Mei, mwaka huu ilipitisha sheria tata ya kupinga mapenzi ya jinsia moja ambayo inajumuisha hukumu ya kifo kwa baadhi ya vitendo vya mapenzi ya jinsia moja.

Hata hivyo, pamoja na haya Rais Museveni aliipongeza Marekani kwa kudumisha ufadhili wa dawa za Virusi vya Ukimwi (VVU), akidokeza kwamba serikali yake ina mpango wa dharura wa kupata dawa hizo ikiwa wafadhili wa kigeni watajiondoa. **BBC**



Baadhi ya watu wakitafuta waathirika kwenye vifusi vya jengo lililopigwa mabomu jana katika mji wa Khan Yunis, kusini mwa ukanda wa Gaza. **PICHA: BBC**

# JKT QUEENS HASIRA KWA ATHLETICO MICHUANO CAF

Na Saada Akida

BAADA ya kupoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Mamelodi Sundowns Ladies kwenye mechi ya kwanza ya hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, Kocha Msaidizi wa JKT Queens, Azishi Kondo, amesema kosa moja tu walilofanya ndilo lililowafanya waadhibiwe, lakini sasa wanajipanga kwa mchezaji ujao.

**Hata hivyo, amekiri kuzidiwa na wapinzani kwa kutumia makosa waliyoyafanya na kupata ushindi huo kwenye mchezo wa kwanza wa michuano hiyo inayoendelea nchini Ivory Coast.**

Akizungumza na Nipashe jana, Kondo (pichani) alisema kwenye kundi lao kuna mechi tano na kwamba baada ya kupoteza mchezo huo wanajiandaa na mchezo mwingine watakaocheza kesho dhidi ya wenyeji wao, Athletico FC d'Abidjan ya nchini humo.

Alisema wanaenda kufanyia kazi makosa yaliyojitokeza ikiwamo safu ya ushambuliaji kutokuwa makini, kwenye mechi iliyopita ambayo walifanikiwa kutengeneza nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia.

"Tunatambua hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu tunakutana na wenyeji wetu, nao wanahitaji kupata matokeo, sasa tunarejea uwanja wa mazoezi kufanyia kazi mapungufu ikiwamo umakini kwa washambuliaji wetu,"



alisema kocha huyo msaidizi.

Naye nyota wa JKT Queens, Joyce Lema, alisema ulikuwa mchezo mzuri na haukuwa rahisi huku akikiri wapinzani wao waliwazidi katika sehemu ndogo na kupata ushindi huo.

"Ulikuwa mchezo mgumu, tulifanya makosa yakatugharimu, benchi la ufundi limeyaona na litafanyia kazi, tunaenda kujiandaa na mchezo ujao kwa ajili ya kutafuta matokeo mazuri," alisema nyota huyo.

JKT Queens wako katika Kundi A ambalo pia linajumuisha wenyeji, Athletico FC d'Abidjan, Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini, Sporting Club Casablanca ya Morocco.

Kikosi cha timu hiyo kinatarajia kushuka dimbani katika mchezo wa pili kesho dhidi ya wenyeji Athletico FC katika Uwanja wa Amadou Gon Coulibaly jijini Korhogo, Ivory Coast.

## Bara, Z'bar U-15 zaanza CECAFA kwa kishindo

Na Adam Fungamwango

TIMU za soka za Tanzania Bara na Visiwani chini ya miaka 15 (U-15), juzi zilianza vema michuano ya Kombe la Afrika Mashariki na Kati, Ukanda wa CECAFA kwa kushinda mechi zao za kwanza, zikichezwa Uwanja wa Njeru, Jinja nchini Uganda.

Wakati Bara iliidungua Somalia bao 1-0, Zanzibar iliichakaza Rwanda mabao 3-0, timu zote hizo zikiwa za Kundi B.

Bao pekee la vijana wa Bara U-15 liliwekwa kambani na Kaniki Selemani na likadumu hadi dakika 90 za mchezo.


Kwa upande wa Zanzibar, mabao yao yalifungwa na Mwinyi Hassan kipindi cha kwanza, kabla ya Mohamed Nassor na Lukuman Omar hawajapachika mabao mengine mawili kipindi cha pili na kuipa ushindi huo ambao unaifanya kuongoza kundi hilo ikiwa na pointi tatu na mabao matatu, ndugu zao wa Bara wakishinda nafasi ya pili kwa pointi tatu na bao moja.

Katika mechi zingine za Kundi A, wenyeji wa michuano hiyo Uganda, wametoa onyo kwa timu zote zinazoshiriki baada ya kuiangamiza Djibouti mabao 15-0.

Kwingineko Timu ya Taifa ya Ethiopia U-15, ililazimishwa sare ya bao 1-1 dhidi ya Sudan Kusini, huku kwa matokeo hayo, Uganda sasa ikiongoza kundi hilo.

Kikosi cha vijana wa Tanzania Bara kitarejea tena dimbani kesho, Jumatano kucheza dhidi ya Rwanda, huku Zanzibar ikicheza dhidi ya Somalia na Novemba 11, mwaka huu kitamalizia mechi zake za makundi dhidi ya ndugu zao wa Zanzibar.

**Katika mechi zingine za Kundi A, wenyeji wa michuano hiyo Uganda, wametoa onyo kwa timu zote zinazoshiriki baada ya kuiangamiza Djibouti mabao 15-0.**




Meneja Masoko wa Tigo, Fabian Felician (katikati), akiwa pamoja na Meneja Masoko wa Parimatch, Levis Paul (kulia) na Justine Lawena wa Tigo wakati wa uzinduzi wa Promosheni ya 'Vibunda Spesho' jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Parimatch, Tigo Pesa waja na 'Vibunda Spesho'

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya Michezo ya Kubashiri ya Parimatch, kwa kushirikiana na Mtandao wa Tigo Pesa, imezindua rasmi Promosheni yake mpya ya 'Vibunda Spesho', yenye lengo mahsusi kuwazawadia wateja wao fedha kila siku na wiki wakati huu wa kuelekea maandalizi ya Sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya.

Kampeni hiyo iliyozinduliwa jana jijini Dar es Salaam, ni mahususi kwa wateja wote wa Tigo Pesa na Parimatch wenye akaunti na hata wapya watakaojiunga katika kipindi cha kuanzia jana Novemba 6 hadi Desemba 6, mwaka huu.

Hayo yamebainishwa na Meneja wa Masoko wa Parimatch, Levis Paul, na kueleza kuwa baada ya kufanya maboresho makubwa katika kutovuti yao kwa kuwapa wateja wao Parimatch Jackpot, sasa hivi wameamua kuwajaza vibunda ili wazidi kuburudika pindi wanapokuwa wanasuka mikeka yao kupitia Parimatch.

"Mteja wa Parimatch akifanya bashiri kwenye mchezo wowote kupitia www.parimatch.co.tz atakuwa na fursa ya kushinda zawadi ya Sh. 50,000, kila siku na kila mwisho wa wiki, yaani siku ya Ijumaa kutakuwa na droo kubwa ya kumtafuta mshindi wa zawadi ya milioni moja ambayo itakuwa inaoneshwa mubashara kupitia Runinga ya TBC," alisema Paul.

Kwa upande wa, Meneja wa Biashara wa Kampuni ya Tigo Pesa, Fabian Felician, amewahimiza wateja wa mtandao huo kuchangamkia fursa kupitia promosheni hiyo ambayo wanashirikiana na Parimatch.

"Wateja wa mtandao wa Tigo Pesa wanaweza kupata zawadi hizo kupitia Parimatch kwa kusuka mikeka yao kwenye tovuti pamoja na App ya Parimatch mara tu unapojisajili endapo ni mteja mpya na kwa wale wenye akaunti, tayari watapaswa kuingia ili waanze kusuka mikeka yao na kusubiria ushindi wao," alisema Fabian.

Kampuni ya Parimatch ndio kinara wa michezo ya kubashiri mtandaoni na imekuwa ikitoa ofa kubwa ya bonasi ya ukaribisho ya asilimia 125 hadi kufikia Sh. 1,000,000 kwa wateja wapya wanaojiunga nao.

Parimatch imekuwa ikifanya kazi nchini Tanzania tangu mwaka 2019, ikitoa huduma nzuri ikijumuisha malipo ya haraka, 'odds' kubwa na promosheni za kusisimua kwenye soka, kasino na michezo ya virtual.

Mbali na soka, kampuni ya Parimatch pia hutoa mamia ya matukio kila siku kwenye tenisi, UFC, mpira wa kikapu, kriketi, baseball na michezo mingine mingi ya 'Live' (mubashara) na pre-match.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### WHITE NYONGEZA KUBWA

ARSENAL iko tayari kumpa mlinzi wa England, Ben White, nyongeza kubwa ya mshahara huku wakitarajia kumwongezea mkataba mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26. ***(Football Insider)***

### ZIELINSKI AWANIWA LIVER

KLABU za Liverpool na West Ham zote zinatazamia kumnunua kiungo wa kati wa Napoli raia wa Poland, Piotr Zielinski mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake unaisha msimu huu wa majira ya joto. ***(Teamtalk)***

### ZAMBRANO ATAKIWA LUTON

KLABU ya Luton bado wana matumaini ya kumnunua kiungo wa kati wa Ecuador mwenye umri wa miaka 19, Oscar Zambrano, mchezaji wa LDU Quito. ***(Sun)***

### ALONSO, SERGI BASI TENA

NYOTA wa Hispania, Marcos Alonso mwenye umri wa miaka 32 na Sergi Roberto mwenye miaka 31, hawatapewa mikataba mipya na Barcelona. ***(Sport)***

### MADRID HAITASAJILI JANUARI

KLABU ya Real Madrid haitafanya usajili mpya katika dirisha la usajili la Januari. ***(Fichajes)***

### KUSAKA NYOTA ULAYA

KOCHA wa Al-Ettifaq, Steven Gerrard, amedokeza kuwa timu yake itavamia Klabu za Ulaya kwa mara nyingine tena Januari kutafuta wachezaji wapya. ***(Goal)***

### LENGLET AZUSHA HOFU

BARCELONA inaaminika kuwa na wasiwasi kuhusu hali ya mlinzi wa Ufaransa aliyepo kwa mkopo pale Aston Villa, Clement Lenglet, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, akiwa bado hajacheza Ligi Kuu England. ***(Sport)***

### VINICIUS KUVUTA NYOTA

KLABU ya Real Madrid inatumaini urafiki ambao fowadi wa Brazil Vinicius Junior mwenye umri wa miaka 23, alionao na nyota wenzake unaweza kuwa ufunguo wa kupata usajili wa baadaye wa wachezaji kama beki wa Canada na Bayern Munich, Alphonso Davies (23), na mshambuliaji wa Paris St-Germain Mfaransa Kylian Mbappe, 24. ***(AS)***

### NARI AMSHAURI MBAPPE

NYOTA wa zamani wa Arsenal, Samir Nasri, amemshauri Kylian Mbappe abaki Ufaransa badala ya kuelekea Real Madrid msimu ujao wa majira ya joto. ***(Le10Sport)***

### SIMEONE MKATABA MPYA

KOCHA Mkuu wa Atletico Madrid, Muargentina Diego Simeone, anakaribia kuongezewa mkataba na klabu hiyo ya LaLiga hadi angalau mwaka 2027. ***(Marca)***

### PAU NA DILI LA MADRID

MLINZI wa Aston Villa na Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 26, amesema alikuwa karibu kujiunga na Real Madrid kutoka klabu ya zamani ya Villarreal msimu wa 2021. ***(Sky Sports)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA ATAKA NYOTA WENYE HASIRA MAN CITY

**MANCHESTER,** England

Nataka Grealish awe na hasira pia acheze vizuri na kisha Doku naye...

KOCHA Pep Guardiola anaamini ni ishara nzuri ikiwa wachezaji wake wa Manchester City "wana hasira" kwa kuachwa nje ya kikosi cha kwanza.

**Jeremy Doku alifunga na kutoa asisti nne katika ushindi wa mabao 6-1 dhidi ya Bournemouth Jumamosi.**

Winga huyo alikuwa kwenye benchi katika ushindi wa wiki iliyopita dhidi ya Manchester United, huku Jack Grealish akianza, lakini majukumu yalibadilishwa wakati wa mchezo wa Jumamosi.

"Nataka Jack (Grealish) awe na hasira na nataka acheze vizuri," alisema Guardiola.

"Na kisha Doku - kuwa na hasira kwamba hajacheza mechi mbili zilizopita. Hii ndiyo njia ya kudumisha uthabiti katika kiwango hicho."

Huku City ikisonga kileleni mwa Ligi Kuu England Jumamosi ikiipita Tottenham Hotspur pointi moja ambapo inacheza leo na Chelsea, na mchezaji wa Kimataifa wa Ubelgiji, Doku aliyesajiliwa kwa pauni milioni 55.4 kutoka Rennes majira ya joto, ameimarika haraka - akifunga mabao matatu katika mashindano yote.

Doku mwenye umri wa miaka 21, anapambania namba na Grealish, ambaye hakutumika kama mchezaji wa akiba wikiendi na bado hajafunga bao kwenye ligi msimu huu.

Guardiola alisema: "Kama vile Jeremy na Jack wanavyofanya na ninaweza kuwachezesha wote wawili kwa wakati mmoja, lakini lazima wanishawishi kwenye mazoezi.

"Jinsi (Grealish) alivyocheza pale Old Trafford, ili kutupa utulivu zaidi na nguvu zaidi katika nafasi hiyo, ilikuwa uamuzi kwetu.

"Tunahitaji kila mtu. Kuna michezo mingi na kila mtu anatakiwa kushindana.

"Basi tutashinda michezo na mtafurahi na kila mtu atafurahi. Hiki ndicho tunachopaswa kufanya."

City itawakaribisha mabingwa wa Uswisi Young Boys katika Ligi ya Mabingwa Ulaya leo Jumanne.




# 'REAL MADRID HAIMTEGEMEI BELLINGHAM'

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti alikanusha kuwa Real Madrid wanategemea zaidi mabao ya Jude Bellingham baada ya timu hiyo kutoka sare ya bila kufungana na Rayo Vallecano kwenye mchezo wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Jumapili.

Sare ya bila kufungana kwenye Uwanja wa Santiago Bernabeu ilikuwa ni mara ya kwanza msimu huu kwa Madrid kushindwa kufunga na kuwafanya wabaki nafasi ya pili kwenye msimamo, pointi mbili nyuma ya vinara Girona.

Bellingham, ambaye amefunga mabao 10 katika mechi 11 za LaLiga msimu huu, alicheza dakika zote 90, lakini jana Jumatatu alitarajiwa kufanyiwa vipimo baada ya kuanguka vibaya katika kipindi cha kwanza na alihitaji matibabu kwenye bega.

"Bellingham alikuwa na tatizo la bega na atafanyiwa tathmini," alisema Ancelotti katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi. "Aliweza kuendelea. Atafanyiwa vipimo, tutegemee si mbaya na anaweza kucheza Jumatano (dhidi ya Braga kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya)."

Ancelotti alisisitiza kwamba Madrid wana wafungaji wa kutosha wa mabao katika kikosi chao kuweza kustahimili iwapo Bellingham hawezi kupata bao, au hayupo.

"Hapana. Tuna rasilimali nyingi," alisema. "Leo (juzi) tumetengeneza nafasi na (Fede) Valverde, pamoja na Vinicius Junior, Joselu na Rodrygo."

Madrid walipiga mashuti 22 dhidi ya Rayo, matano yakilenga goli, lakini hawakuweza kupata matokeo.

"Tulijaribu kwa krosi, tulijaribu kupitia mipira, tulijaribu kwenda moja kwa moja, tulijaribu kila njia na haikufanikiwa," aliongeza Ancelotti.

"Kila mtu anajua inaweza kutokea. Lazima uamini hadi mwisho, na wachezaji walijaribu hadi sekunde ya mwisho.

# Diaz aomba watekaji wamwachie baba yake




**LIVERPOOL,** England

NYOTA wa Liverpool raia wa Colombia, Luis Diaz amewasihi watekaji nyara wa baba yake wamwachilie mara moja na "kumaliza kusubiri kwa maumivu".

Wazazi wote wawili wa Diaz walikamatwa wakiwa wamenyooshewa bunduki katika mji aliozaliwa wa Barrancas na waasi wa mrengo wa kushoto wa Jeshi la Ukombozi la Kitaifa (ELN) Oktoba 28, mwaka huu.

Wakati mama yake alipatikana, baba yake bado hajaachiliwa.

Diaz alifunga bao dhidi ya Luton Jumapili na akaiinua jezi yake kuonesha maneno kwa Kihispania "uhuru kwa baba".

"Kila sekunde, kila dakika wasiwasi wetu unaongezeka," alisema Diaz mwenye umri wa miaka 26, katika taarifa iliyotolewa muda mfupi baada ya mechi ya Ligi Kuu England.

"Mama yangu, mimi na kaka zangu tumekata tamaa, tunahangaika na hatuna maneno ya kuelezea kile tunachohisi, mateso haya yataisha tu tukiwa naye nyumbani.

"Naomba wamwachilie mara moja, wakiheshimu uadilifu wake na kukomesha kusubiri huku kwa maumivu. Kwa jina la upendo na huruma tunaomba wafikirie upya matendo yao na kuturuhusu kumpata tena."

# Marcelo akunwa na Libertadores

**RIO DE JANEIRO,** Brazil

MARCELO amesema kutwaa Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini), akiwa na Fluminense ni "muhimu" zaidi kwake kuliko mataji matano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya aliyoshinda akiwa na Real Madrid baada ya klabu hiyo ya Brazil kushinda dhidi ya Boca Juniors, Juzi.

Beki huyo wa kushoto aliichezea Fluminense kwa dakika 80 - klabu ambayo aliihama kwenda Madrid akiwa kijana mwaka 2007, kabla ya kujiunga tena mapema mwaka huu - katika ushindi wa mabao 2-1 kwenye muda wa ziada Uwanja wa Maracana mjini Rio de Janeiro.

John Kennedy aliyetokea benchi na kufunga bao la ushindi dakika ya 99 - baada ya Luis Advincula kuisawazishia Boca kufuatia Mjerumani Cano kufunga bao la kwanza - kabla ya kutolewa kwa kadi nyekundu dakika mbili baadaye.

Marcelo anashikilia rekodi ya mchezaji aliyeshinda mataji mengi zaidi kwa Real Madrid (25), katika kipindi cha miaka 15 alichokaa hapo.

"Real Madrid wataelewa," alisema. "Ni taji langu muhimu zaidi, katika ngazi ya klabu, kwa sababu ni klabu iliyonilea. Real inajua daima iko moyoni mwangu. Ni vigumu kusema. Ni furaha maradufu."

Marcelo aliondoka Madrid kwa uhamisho wa bure msimu wa majira ya joto wa 2022 baada ya kushinda taji lake la tano la Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Liverpool huko Paris.

Ushindi wake wa mataji 25 ni pamoja na Ligi ya Mabingwa mara tano, Klabu Bingwa ya Dunia mara nne, UEFA Super Cups mara tatu, mataji sita ya LaLiga, Copas del Reys mawili na Supercopa mara tano.

Alijiunga na Olympiakos ya Ugiriki kwa uhamisho wa bure Septemba 2022, lakini alicheza mechi 10 pekee kabla ya kukatisha mkataba wake miezi mitano baadaye na kujiunga tena na Fluminense Februari 2023.



HABARI MICHEZO

# NBC YAJA NA 'SOKA LIMEITIKA' IKIFURAHIA 'DABI' YA KARIAKOO

Na Mwandishi Wetu

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), ambayo ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu ya Soka ya Tanzania Bara (NBC Premiere League) juzi ilinogesha shangwe za mechi ya watani wa jadi ('Dabi' ya Kariakoo), Simba na Yanga kwa kuwapeleka uwanjani wateja wake pamoja na wadau mbali mbalimbali wa benki hiyo ili kushuhudia mtanange huo ulioisha kwa timu ya Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 5 -1.

Aidha, benki hiyo pia iliandaa matukio mbalimbali kwa ajili ya mashabiki wa soka pamoja na wateja wake katika maeneo mbalimbali ya jijini Dar es Salaam na Mwanza, huku pia ikitumia mechi hiyo kubwa kuzindua rasmi kampeni maalum ya msimu wa huu wa soka inayofahamika kama 'Soka Limeitika' ambayo inalenga kuhamasisha na kujivunia mafanikio ya mchezo huo kutokana na udhamini wake kwenye ligi hiyo.

**Katika tukio kubwa lililofanyika Hotel ya Hyatt Regency, Dar es Salaam, ilishuhudiwa Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi, akiongoza hafla fupi ya chakula cha mchana maalum kwa ajili ya baadhi ya wateja wakubwa na wadau wengine wa NBC, tukio lililofuatiwa na msafara maalum kuelekea Uwanja wa Benjamin Mkapa kushuhudia mechi hiyo.**

"Tumetumia mechi hii kubwa ili kwa pamoja tuweze kujumuika na kufurahia sambamba na wadau wetu hawa muhimu. Lengo ni kupata wasaa mzuri ili kufurahia pamoja ile ladha ya mchezo huu pendwa.

"Wote kwa pamoja tutakwenda uwanjani katika msafara maalum na baada ya mechi tutarudi pamoja kutoka uwanjani hadi hapa hotelini kisha tutaachana huku kila mmoja akienda kwake akiwa salama kabisa," alibainisha Sabi.

Akizungumzia kwa kina kuhusu Kampeni ya 'Soka Limeitika', Meneja Masoko wa NBC, Alina Kimaryo, alisema mbali na kuhamasisha ari ya mchezo huo pendwa, kampeni hiyo inalenga kujivunia mafanikio ya mchezo huo yaliyopatikana kutokana na udhamini wa NBC kwenye ligi hiyo inayozidi kujiongezea umaarufu barani Afrika na ulimwengu kwa ujumla.


"Tangu tuwekeze nguvu kwenye ligi hii Benki ya NBC na wadau wa mchezo wa soka tumeshuhudia mafanikio mengi ya kujivunia ikiwamo kuongezeka kwa ubora wa ligi yetu kitaifa na kimataifa ambapo nafasi ya ubora wa ligi yetu kwa viwango vya bara la Afrika kwa sasa ni nafasi ya tano kutoka ya 12 tuliyoikuta wakati tunaanza udhamini wetu.

"Pia udhamini wetu umeziongezea uwezo wa kiuchumi klabu zinazoshiriki ligi hii na sasa zipo imara kwenye eneo hilo na ndio sababu sasa hata mechi zinafanyika kulingana na ratiba bila klabu kukwama kufika viwanjani kutokana na ukata," alibainisha.

Aidha, alitaja mafanikio mengine kuwa ni pamoja na utoaji wa bima za afya kwa wachezaji, familia zao na bechi la ufundi, mikopo ya mabasi inayoendelea kutolewa na benki hiyo kwa klabu mbalimbali zinazoshiriki ligi hiyo, ubora wa viwanja, udhamini wa NBC Championship na Ligi ya Vijana (Youth League) sambamba na uboreshaji wa huduma ya mauzo ya tiketi za michezo ya ligi hiyo kupitia mawakala wa NBC waliopo maeneo mbalimbali nchini.

"Ni wazi kwamba udhamini wa NBC umeongeza vipato kwa klabu ndio sababu sasa tunashuhudia zikiweza kusajili kwa ushindani wachezaji bora kutoka ndani na nje ya nchi hatua ambayo inaziwezesha kufanya vizuri zaidi kwenye mashindano ya ndani na yale ya kimataifa.

"Hamasa hii inayoshuhudiwa sasa kwenye mchezo huu pia ni matunda ya udhamini wa NBC na hiyo ndio maana halisi ya 'Soka Limeitika,' Alia alihitimisha.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NBC, Theobald Sabi (kushoto), akibadilishana mawazo na wateja pamoja wadau wao mbalimbali wakati wa hafla ya chakula cha mchana iliyoandaliwa na benki hiyo kwa ajili ya wateja wake wakubwa kabla ya kuelekea Uwanja wa Benjamin Mkapa kushuhudia mechi ya 'Dabi' ya Kariakoo kati ya Simba na Yanga iliyoisha kwa Yanga kuibuka na ushindi wa mabao 5 -1. **MPIGAPICHA WETU**

## *Namungo na hesabu kali kuivaa Simba SC*

Na Saada Akida

KOCHA wa Namungo FC, Denis Kitambi, ameanza kuipigia mahesabu Simba, akisema anawaandaa wachezaji wake kwa mchezo huo mgumu utakaochezwa keshokutwa, Alhamisi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Amesema hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu ya wapinzani wanaokwenda kukutana nao ambao wametoka kujeruhiwa, hivyo ni lazima wawe makini katika safu ya ulinzi kuelekea mchezo huo.

Namungo FC wako mjini wakiendelea kujiimarisha ili kuwakabili Simba katika mchezo huo.

Akizungumza na Nipashe jana, Kitambi alisema kikubwa anaendelea kufanyia kazi mapungufu ya kikosi chake, kuwahimiza mabeki wake kuwa makini na safu ya ushambuliaji ya Simba ambayo tangu kuanza kwa msimu huu haijawahi kutoka uwanjani bila kucheka na nyavu.

Alisema licha ya Simba kupoteza mechi ya juzi, wataingia kwa tahadhari kubwa kwa sababu ya kutafuta alama muhimu na anaimani wapinzani wao watakuja kivingine kumaliza hasira zao.

"Maandalizi yapo safi, mpaka sasa wachezaji wote wapo vizuri, Kikubwa ni kumheshimu mpinzani wetu na vijana kujituma, hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu ya matokeo ya wapinzani wetu kupoteza mechi yao iliyopita.

Simba ni timu kubwa ina wachezaji wazuri hata ukiangalia safu ya ushambuliaji iko imara lakini wana mapungufu kwenye ulinzi ninaimani vijana wakipambana tunaweza kupata alama muhimu," alisema kocha huyo.

## *Simba watoa sababu kukubali kipigo Yanga*

INATOKA UKURASA 24

msimu huu.

"Mechi ilikuwa ngumu na yenye presha sana, jambo zuri ni kwamba tumeshinda mabao 5-1, lakini sasa tunatakiwa kusahau haya matokeo na kuomba Mungu kusaidia kufanya vizuri katika michezo yetu ijayo, kumfunga Simba ni kuweka heshima tu, kazi kubwa kutafuta ubingwa," alisema Nzengeli.

**MANAHODHA SIMBA, YANGA**

Nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, yeye alishangazwa na timu ya Simba kuruhusu mabao mengi kirahisi katika mechi ya dabi, kitu ambacho hakukitarajia.

"Ni ushindi mkubwa kama ukubwa wa mechi yenyewe, dabi imechezeka, lakini ndiyo kama hivyo mpinzani wetu karuhusu mabao mengi zaidi kwa hiyo dabi imekosa kidogo uzuri na ule utamu wake kwa sababu haikuwa na mzani sana kama siku zote, lakini kwetu sisi tunajipongeza.

"Katika mechi hii wakati wa mapumziko tukiwa bao 1-1, tuliambizana ndani kwamba wapinzani wetu wameshapata bao, basi tulinde kwanza tusiwe na haraka ya kwenda mbele kuwashambulia maana Simba ni timu kubwa ujue kama ilivyo sisi hapa tuliambizana tutulie kwanza kama ni mabao tutayapata baadaye na kweli ikawa hivyo.

Naye Nahodha Msaidizi wa Simba, Mohamed Hussein 'Tshabalala', alisema mpinzani wao alikuwa bora na waliingia wakiwa na mfumo tofauti na ule uliozoeleka, hivyo wakawachanganya.


"Nafikiri tumejitahidi kucheza kwa maelekezo ya mwalimu, lakini nafikiri 'plani' haikufanya kazi, ila maelekezo yalikuwa kama tulivyotakiwa kuyafanya, nadhani mpinzani wetu alikuwa bora zaidi na ameweza kutuadhibu.

"Wenzetu walikuwa na plani ya kuwa na viungo wengi katikati ya uwanja na hicho ndicho kilichotuvuruga kwa sababu kila mtu anafahamu aina yao ya uchezaji ni watu wanaotumia zaidi mawinga, lakini leo hawakucheza hivyo, hawakuwa na mawinga asilia, walikuwa na mawinga viungo, hilo ndilo lililotuchanganya, wakawa wengi kati, plani yetu ikafia hapo na tulichelewa kulitambua, baadaye walimu walilitambua hilo tukarekebisha pamoja na hayo tukaambulia matokeo mabaya," alisema Tshabalala.

# Michezo

Jumanne Novemba 7, 2023

Nipashe

Marcelo akunwa na Libertadores UKURASA 22



Wachezaji wa Yanga wakishangilia kwa ishara ya kuonyesha mkono wakiwa na maana ya mabao matano waliyoifunga Simba wakati wakishinda 5-1 katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Simba watoa sababu kukubali kipigo Yanga

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

## Gamondi atamba, Robertinho ajitetea huku Wanasimba wakisema sawa lakini ni kikubwa sana...

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga Miguel Gamondi akisema ushindi wa mabao 5-1 walioupata dhidi ya Simba juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam hauwezi kuamua kitu chochote kuelekea kwenye ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha wa Simba, Robertinho Oliveira, amesema kipigo hicho ni sehemu ya soka na kuongeza kuwa wachezaji wake walipoteza umakini wa kuzuia kipindi cha pili.

**Hata hivyo, wakati makocha hao wakisema hayo, Mjumbe wa Baraza la Ushauri la Klabu ya Simba, Geofrey Nyange 'Kaburu', amesema timu yao imecheza ovyo na matokeo hayo hayaleti picha nzuri kwenye klabu hiyo, huku Ismail Aden Rage akiwasifu Yanga kwa kufanya usajili mzuri wa wachezaji bora na vijana.**

Katika mchezo huo mabao ya washindi, mawili yalifungwa na Maxi Nzengeli, Kennedy Musonda, Stephane Aziz Ki na Pacome Zouzoua, huku bao pekee la Simba likifungwa na Kibu Denis akiunganisha kona ya Saido Ntibazonkiza.

"Kipindi cha kwanza Simba walikuwa vizuri, dakika 45 ya kipindi cha pili niliwaeleza wachezaji wangu kucheza mpira, kuhusu ubingwa sasa ni mapema sana kuzungumzia, ushindi huu huuwezi kuamua kitu katika mbio za ubingwa.

"Tunatakiwa kupambana kushinda kila mchezo uliyopo mbele yetu na sasa tunarejea katika uwanja wa mazoezi kujiandaa na mchezo wetu ujao," alisema Gamondi.

Kwa upande wa Kocha Mkuu wa Simba, Robertinho alisema kipigo cha mabao 5-1 walichokipata kutoka kwa watani wao, Yanga ni sehemu ya mpira.

Alisema kipindi cha pili walipoteza umakini na kushindwa kuzuia nafasi ambazo wapinzani wao ambao walizitumia vizuri.

"Hatukuwa vizuri wakati wanapopoteza mpira na wapinzani walitumia mwanya huo.

"Nawapongeza wapinzani kwa ushindi hatukuwa vizuri hasa kipindi cha pili baada ya kumpoteza Kibu uwanjani, lakini huu ni mpira na tunajipanga kwa mchezo ujao," alisema Robertinho.

**KABURU, RAGE**

Naye Kaburu alisema anakubali kufungwa na mtani wake Yanga, lakini mabao matano ni mengi sana.

"Niwapongeze Yanga kwa ushindi, goli tano ni nyingi na ni nyingi sana, nadhani viongozi wataongea, mimi kama mwanachama na shabiki nimeangalia mpira tumecheza ovyo tumefungwa, tumekubali matokeo, viongozi watajipanga. Tumecheza ovyo," alisema Kaburu.

Mjumbe mwingine, Rage yeye alisema timu yake imefungwa mabao mengi, na anachokiona ni kwamba Simba haikuwa makini kwenye usajili, huku akiisifu Yanga kwa kufanya usajili bora wa maeneo yenye mapungufu, lakini ikiwa na wachezaji wengi vijana.

"Mara ya mwisho kuifunga mabao 5-0 Yanga mimi ndiyo nilikuwa kiongozi Simba, nadhani tatizo hatukuwa makini kwenye usajili, wenzetu wana timu nzuri na wachezaji wao wengi ni vijana sasa," alisema Rage.

**NZENGELI**

Mfungaji wa mabao mawili kwenye mechi hiyo, Nzengeli alisema bado wana kazi kubwa ya kufanya katika michezo iliyopo mbele yao na watahakikisha wanashinda na kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara

INAENDELEA UKURASA 23

## Kipigo Simba SC gumzo bungeni

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KIPIGO cha timu ya Simba dhidi ya Yanga jana kimekuwa gumzo bungeni kikichagizwa na ishara za wabunge kumpungia mkono Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson.

Yanga iliichapa Simba mabao 5-1 katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Jana bungeni Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba ambaye anadaiwa kuwa mwanachama na shabiki mkubwa wa Yanga, alipokaribishwa kuwasilisha mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25, alimpungia mkono Spika kuashiria magoli matano waliyoifunga Simba juzi, huku wabunge wengine wakishangilia.

Aidha, alipomaliza kuwasilisha mpango huo alimpungia tena spika mkono mmoja ishara ya kuondoka jambo lililomfanya spika na wabunge kucheka.

Kutokana na hali hiyo, Spika Tulia alisema "Waheshimiwa wabunge nilikuwa natafakari hapa, kumbe napungiwa mkono kuonesha kwamba jana Yanga wamefunga magoli matano".

Hata hivyo, aliipongeza Yanga kwa mpira mzuri waliocheza juzi uliowafanya kupata ushindi huo.

"Sawa tunawapongeza Yanga kwa mpira mzuri waliocheza jana, sasa si mnajua kanuni zetu nikishasema hapa mbele, nishasema kwa niaba ya bunge ndio kanuni zetu zinavyosema msianze kuleta fujo huku bungeni," alisema Spika Tulia.

Katika mchezo huo mabao ya washindi, mawili yalifungwa na Maxi Nzengeli, Kennedy Musonda, Stephane Aziz Ki na Pacome Zouzoua, huku bao pekee la Simba likifungwa na Kibu Denis akiunganisha kona ya Saido Ntibazonkiza.

Ushindi huo unaifanya Yanga kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu Bara ikiwa na pointi 21 baada ya michezo nane huku Simba yenye mechi moja mkononi ikishika nafasi ya tatu kwa alama zake 18.

Azam FC ndiyo inayoshika nafasi ya pili kwa pointi zake 19, lakini michezo miwili mbele dhidi ya Simba na mmoja mbele dhidi ya Yanga.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042